**Matukio** ya moto shule za taasisi za dini yamshtua Rais Samia

UKURASA 2



**Dk. Mwinyi** acharuka ataka uchunguzi wizi fedha za umeme

UKURASA 5




UKURASA 11


# Nipashe

Jumatatu Julai 12, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580639

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Maswali magumu 5 moto wa Kariakoo

• **LAUNGUA** siku ya kumbukumbu ya mbunifu wake, 1,662 waathirika, Samia awapa pole, PM atoa siku 7...

*Endelea ukurasa 2 & 3*



Soko la Kariakoo lililoungua moto juzi usiku na kuteketeza maduka yaliyokuwa ndani yake, likiwa limegubikwa na moshi hadi jana. **PICHA: MIRAJI MSALA**

# Barakoa lazima sokoni, 'level seat' daladala

UKURASA 4

## Askofu Malasusa: Msipende umaarufu kupitia misaada

UKURASA 4

**MICHEZO** **YANGA YAELEKEZA NGUVU FAINALI FA** UK.24

**MAONI, KATUNI** UK.6




Mkazi wa Kijiji cha Kizito Wonjwa, Kimbiji -Kigamboni akiwa amebeba maji aliyochota katika bomba jipya baada ya kukabidhiwa na Kampuni ya Davis & Shirtliff (D&S) Group Jumamosi. Nyuma ni Ofisa Tarafa wa Pemba Mnazi, Florence Msigwa, viongozi wa mitaa, wafanyakazi wa D&S na wakazi wa kijiji hicho wakifurahia. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Maswali magumu 5 moto wa Kariakoo

**Na Christina Mwakangale**

MASWALI magumu yameibuka juu ya namna Jeshi la Zimamoto na Uokoaji lilivyokabili tukio la moto kwenye soko la kihistoria la Kariakoo, jijini Dar es Salaam na chanzo halisi.

Maswali hayo ni pamoja na umbali wa yalipo Makao Makuu ya Zimamoto (Fire) Upanga, Dar es Salaam na Soko la Kariakoo, ambao ni kilomita moja.

Jingine ni muda uliotumiwa katika kudhibiti moto huo ambao ulizuka kuanzia saa 2:40 juzi usiku na udhibiti ulikwenda hadi saa 9 usiku.

Jingine ni uwapo wa miundombinu ya maji ya kuzima moto kwa eneo la Kariakoo, kwa kuwa magari yalipoishiwa maji yalikosa pa kuongezea maji na kulazimika kuyafuata mbali.

Jingine ni muda tukio lilipotokea ni ambao hakuna foleni wala watu wengi hivyo ni rahisi kwa magari ya Zimamoto kufika kwa wakati na kuudhibiti, lakini hayakufanikiwa kufanya hivyo.

Jingine ni uwezo wa Zimamoto kukabili matukio kwa haraka kabla ya kusababisha madhara makubwa, na kama wana vifaa vya kuhimili matukio hasa kwa maeneo kama Kariakoo yenye maghorofa mengi yaliyobanana.

"Ikiwa Zimamoto wako umbali usiozidi kilomita moja hadi soko lilipo wameshindwa kufika mapema na kudhibiti moto huu, ikiwa hakuna miundombinu ya maji katika eneo muhimu kama hili ambalo ni kitovu cha uchumi wa nchi, hii ni hatari sana inazua maswali magumu," alisema Joseph Kavishe.

Aidha, alionyesha kushangazwa na kukosekana kwa miundombinu na vifaa vya kuzimia moto katika eneo lililotumiwa na wafanyabiashara zaidi ya 224, huku kukiwa na ofisi yenye wafanyakazi wa umma.

Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, jana alitembelea soko hilo na kutoa siku saba za uchunguzi wa tukio hilo na kukabidhi ripoti kwa hatua zaidi.

**SAMIA AWAPA POLE**

Aidha, Rais Samia Suluhu Hassan, ametuma salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla na wafanyabiashara wa Soko Kuu la Kariakoo kufuatia hasara kubwa waliyoipata kutokana na soko hilo kuungua moto, na kuagiza vyombo vya ulinzi na usalama kuchunguza kwa kina kujua chanzo.

"Soko la Kariakoo licha ya kuajiri wafanyabiashara wengi, lakini ni kitovu cha biashara kwa nchi za Afrika Mashariki, hivyo tukio hilo si hasara kwa wafanyabiashara tu bali hata kwa serikali," alisema Rais Samia katika taarifa iliyotolewa na Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu.

**TUKIO HALISI**

Nipashe ilifika jana kwenye soko hilo na kukuta maduka pembezoni mwa soko yakiwa yamefungwa na kuwapo idadi ndogo ya wauzaji na wanunuzi tofauti na siku zote huku vikosi vya ulinzi na usalama vikiimarisha ulinzi.

Mbali na vikosi vya uokoaji na zimamoto vya umma na binafsi kuiambia Nipashe kwamba udhibiti wa moto ili kupunguza madhara ulikuwa ni wa asilimia 90, gazeti hili lilishuhudia moshi mweusi ukiendelea kusambaa eneo la soko, ulio na harufu kali.

Makamu Mwenyekiti wa Machinga Taifa na Wajasiriamali Wadogo, Stephen Lusinde, alisema takribani wafanyabiashara 1,662 wameathiriwa na tukio hilo na kwamba soko hilo ni kati ya masoko yenye historia tangu mwaka 1968.

Alisema takwimu za Shirika la Masoko Kariakoo zinaonyesha wafanyabiashara waliopo ndani ya soko hilo na wanaolipia kodi ya pango ni 224, kati yao waliopo eneo la chini kabla ya kupanda ghorofa ni 120, ghorofa ya kwanza ni 100 na wengine wanne ambao wapo katika matangazo.

"Tukio hili ni kubwa kwa sababu limepiga eneo la kitovu cha soko hili Tanzania, nawapa pole wafanyabiashara wenzetu ambao ni wa aina tatu, wadogo, kati na wakubwa. Yaani wote katika makundi haya wanauziana bidhaa kutoka muuzaji mkubwa hadi mdogo," alisema Lusinde.

"Natoa wito kwa wafanyabiashara wenzangu tuvumilie na Waziri Mkuu Kassimu Majaliwa alifika hapa na kutuambia tuvumilie ndani ya siku saba ili kujua sababu na chanzo," aliongeza Lusinde.

Mmoja wa wafanyabiashara aliyejitambulisha kwa jina la Amina Greyson, alisema amefanya biashara soko hilo tangu mwaka 1997, na kwamba hukopa benki ili kukuza biashara yake hivyo hasara aliyoipata anawaza ni namna gani ataifidia.

**ZIMAMOTO**

Kamishna Jenerali wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, John Masunga, aliiambia Nipashe kwamba baada ya tukio hilo kutokea majira ya saa 2: 40 na kupata taarifa kwenye kituo cha jeshi hilo Ilala, kwa kushirikiana na vikosi vingine walianza kuzima moto.

Alisema hadi saa 8:30 usiku wa manane walifanikiwa kuuzima moto akisema tatizo kubwa walilokumbana nalo ni uhaba wa maji eneo la Kariakoo na kukwamisha kwa kiasi ya utendaji kazi.

"Hakuna mtu aliyejeruhiwa kwa sababu tukio lilitokea usiku pengine lingetokea mchana ingekuwa taharuki na watu kujeruhiwa. Kanuni zetu baada ya kuzima moto ni uchunguzi, uchunguzi utakapokamilika taarifa itatolewa.

Shughuli za biashara zitaendelea kusitishwa itategemeana na ukaguzi na kujiridhisha kwamba lini shughuli zitaendelea," alisema Kamanda Masunga.

Sadiki Mwambambale, mmoja wa waokoaji kutoka kampuni binafsi ya Zimamoto na Ukoaji ya PMM, alisema walifika saa 5 usiku (juzi) eneo la tukio kutoa ushirikiano kuzima moto huo ambao hadi jana ulidhibitiwa kwa asilimia 80 na kwamba umeathiri zaidi eneo la chini la jengo.

"Huko ndani kilichopona hakuna labda majengo na biashara kuzunguka jengo, ATM ya Exim Benki na Benki ya Stanbic. Inasemekana chanzo kikawa ni hitilafu ya umeme. Ila wafanyabiashara na uongozi uangalie wasiache biashara zikakaa bila mpangilio, mfano mtu anayeuza dawa za mimea, mifugo utakuta huyo huyo na cherehani.

"Utakuta pembeni tu kuna biashara ya chakula, majembe, matoroli, maplasiki, imeleta tabu kwetu kuudhibiti mapema moto kutokana na kwamba lazima tuchukue tahadhari za kiafya, ndio maana moshi unaotoka harufu umejaa dawa na plastiki."

## Matukio moto shule taasisi za dini yamshtua Rais Samia

**Na Idda Mushi,** MOROGORO

MATUKIO ya moto ya mara kwa mara kwenye shule zinazomilikiwa na Jumuiya za dini nchini, yamemshtua Rais Samia Suluhu Hassan, na kuviagiza vyombo vya ulinzi na usalama kushirikiana na jumuiya hizo kutafuta vyanzo na kuyadhibiti ili yasijirudie.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi wa Mawasiliano ya Rais, Ikulu, Jaffar Haniu, alisema Rais ametuma salamu za pole kwa Mkuu wa Mkoa, Martin Shigella na Jumuiya za Kiislam Tanzania kutokana na tukio la moto kwa Bweni la Shule ya Sekondari ya Kiislam ya Wasichana AT Town, Manispaa ya Morogoro.

Aidha, kufuatilia matukio hayo Julai na Septemba mwaka jana, Waziri Mkuu, Kassimu Majaliwa, akizungumza katika Baraza la Eid katika viwanja vya Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam, alisema serikali imeunda tume kuchunguza matukio ya moto na alimwagiza aliyekuwa Mkuu wa Mkoa Dar es Salaam, Abubakar Kunenge (kwa sasa RC Pwani), kuunda kamati ya uchunguzi, na baadaye yalitokea mikoa ya Kilimanjaro na Kagera.

Mkoani Morogoro Shule ya Sekondari ya Charlotte iliyopo kata ya Tungi na Shule ya Sekondari ya wasichana inayomilikiwa na Taasisi ya Kiislam ya At-Taaun Islamic Girls Seminary iliyopo kata ya Mwembesongo, ziliteketea kwa moto huku Jeshi la Zimamoto na Uokoaji likiwatahadharisha wamiliki kukagua mifumo ya umeme ili kuhakikisha iko sawa na kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza.

Kamanda wa Zimamoto na Uokaji mkoani Morogoro, SACF Goodlucky Zelote, alisema hayo wakati wa zoezi la uzimaji wa moto mkubwa uliochoma jengo la ghorofa lenye bweni la wanafunzi juu na msikiti chini, katika Shule ya Sekondari ya Wasichana na At Taaun, uliolipuka Julai 10, majira ya saa tatu usiku, na kuweza kudhibitiwa majira ya saa tano usiku. "Asubuhi tumezima tena moto shule nyingine ya Charlotte hapa hapa Morogoro Mjini, ndio maana tunatadhaharisha shule kuchukua hatua kulinda miundombinu yao na usalama wa wanafunzi na watumiaji wengine wa majengo yao," alisema SACF Zelote.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Morogoro, SACP Fortunatus Musilim, alisema bweni hilo liliteketea lilikuwa la wanafunzi 102, na kwamba wako salama na wamepata hifadhi kwenye msikiti ulio jirani na shule hiyo na ulinzi na usalama umeimarishwa kuhakikisha hakuna athari zozote zinazoweza kujitokeza ikiwamo wizi kutoka kwa watu wanaoweza kutumia janga la moto kufanya uhalifu.

Akasema hakuna madhara makubwa ya kibinadamu yaliyojitokeza kutokana na moto huo, isipokuwa wanafunzi sita walikimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Morogoro baada ya kuanguka kutokana na mshtuko.

Mkuu wa shule hiyo, Iddi Suleiman Juma, alisema shule ilifunguliwa Jumatatu na kwamba bweni lina uwezo wa kuchukua wanafunzi 120, isipokuwa ni 102 ambao ni wa bweni ndio walikuwa wamewasili kuanza masomo.

"Inadaiwa moto ulianza kuwaka majira ya saa 2 kama na nusu usiku, lakini ulipamba moto majira ya saa 3 na nusu usiku, wakati huo wanafunzi wengi walikuwa nje, wengine wengi walikuwa msikitini," alisema Mkuu huyo wa shule.

Alibainisha bweni na vifaa vyote vya wanafunzi vimeteketea kabisa. Katika Sekondari ya Charlotte, moto uliteketeza bweni wanalolala wanafunzi wa kike wa kidato cha kwanza sambamba na vifaa vyote vilivyokuwamo ndani yake, ambapo Mkuu wa Shule hiyo, Sista Agness alisema walibaini uwapo wa moto wakati tayari moto ukiwa umepamba majira ya asubuhi, Julai 10.

Baadhi ya wanafunzi wa Charlotte, Mora Michael na Glory Gaspar ambao ni viongozi wa bweni, walisema wanafunzi wote wako salama na kushukuru Jeshi la Zimamoto na Uokoaji kwa kuwahi eneo la tukio na kudhibiti moto huo ili usisababishe madhara zaidi.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (TAMISEMI), Prof. Riziki Shemdoe, alitembelea shule hizo na kuwataka wakuu wa shule kuweka vifaa vya uzimaji wa moto na kuchunguza mabweni na maeneo mengine kuona kama kuna hatari zozote za moto ili kudhibiti mapema na kuondoa hatari zinazoweza kujitokeza.

**MATUKIO YA MOTO**

Hili ni tukio la nne kwa shule zinazomilikiwa na Jumuiya hiyo, ikikumbusha matukio mfululizo wa matukio ya moto katika shule ya Kiislam ya Msingi ya Byamungu, mkoani Kagera yaliyotokea mwaka jana, Julai 18, Julai 23 na tukio la Septemba 13, na matukio ya mkoani Kilimanjaro na mawili Kunduchi na Ilala, Dar es Salaam.

## HABARI KITAIFA

# Soko Kariakoo lilipoungua siku ya kumbukumbu ya mbunifu wake

**Na Salome Kitomari**

SOKO maarufu la kihistoria la Kariakoo limeungua siku na mwezi unaofanana na aliyofariki dunia mbunifu wa jengo hilo, Beda Jonathan Amuli.

Mbunifu huyo alifariki dunia Julai 10, 2016 ikiwa ni miaka sita imepita tangu kifo chake na soko hilo kuungua Julai 10, 2021.

Soko hilo lililopo kitalu namba 32 zone III, lilianza wakati wa utawala wa kikoloni wa Ujerumani, wakati huo Tanzania ikiitwa Tanganyika.

Eneo lililopo soko hilo lilijengwa jengo la utawala wa Wajerumani lililokusudiwa kutumika kama ukumbi wa kuadhimishwa na kutawazwa kwa Mfalme Kaiser Wilheim wa Ujerumani wakati huo.

Kumbukumbu ya soko hilo imeandikwa kwenye mtandao wa Wikipedia, kuwa baada ya Vita Kuu ya Dunia na Waingereza kuuteka mji wa Dar es Salaam, walitumia jengo hilo kama kambi ya jeshi kwa askari wao waliojulikana kama 'carries corps' yani wabeba mizigo inatamkwa 'Karia-koo' na ndiyo chanzo cha kuzaliwa jina la Kariakoo.

Baada ya vita kuu ya kwanza ya dunia kwisha mwaka 1919, Tanzania ilitawaliwa na Waingereza na soko hilo lilianza kutumika kama la kuhudumia wakazi wa jiji wakati huo wafanyabiashara waliuza bidhaa sakafuni hadi miaka ya 1960 meza za saruji zilipojengwa.

Soko hilo halikuwa na ghala za kuhifadhia bidhaa jambo lililowafanya viongozi kuona haja ya kuwa na soko kubwa na la kisasa kulingana na maendeleo ya jiji na uamuzi ulifanywa na serikali mwaka 1970.

"Serikali iliagiza Halmashauri ya Jiji la Dar es Salaam kujenga soko jipya la kisasa ambalo lingechukua nafasi ya soko la zamani, ambalo lingetosheleza mahitaji yao kwa muda wa miaka 50 hadi 70 ijayo kuhusu mambo yote ya vyakula, yaani uuzaji jumla, mahala pa kuhifadhi vyakula na uuzaji wa rejareja," Meneja Mkuu wa Shirika la Masoko Kariakoo, Hetson Kips, alimfafanulia mwandishi wetu aliyekuwa anafanya habari ya uchunguzi wa soko hilo mwaka 2018.

Mchora ramani Marehemu Beda Amuli (aliyefariki Julai 10, 2016), aliandaa ramani iliyokubaliwa na wajenzi waliojenga soko hilo, Mwananchi Engineering and Contracting Company (MECCO) wakisaidiana na makandarasi wengine, na ujenzi uligharimu Sh. milioni 22. "Soko lilifunguliwa rasmi kwa matumizi ya wananchi Desemba 8, mwaka 1975 na Rais wa kwanza wa Tanzania Mwalimu Julius Nyerere," ilisema taarifa hiyo.

Soko hilo lilianzishwa kwa Sheria ya Bunge Na.36 ya mwaka 1974 na matumizi yake yalikuwa ni kupokea mazao ya wakulima kutoka mikoa mbalimbali nchini na kuuza kwa wanunuzi wa masoko mengine wa jumla na rejareja.

Mwonekano wa soko la Kariakoo lililo chini ya Shirika la Masoko Kariakoo (SMK) uliobeba mvuto wa aina yake kama masoko ya Accra-Ghana na Lusaka Zambia, ulilifanya soko hilo liwe la kipekee Afrika Mashariki.

**WANAHISA**

Mwaka 1985 hisa ziligawanywa, Jiji la Dar es Salaam lilichukua asilimia 61 na serikali asilimia 49, lakini hadi mwaka 2018 Nipashe ilivyofanya uchunguzi wa namna soko hilo linavyokufa, cheti cha mwanahisa kilichokuwapo kilikuwa ni cha Hazina pekee, jiji halikuwa na cheti ingawa ni mmiliki mwenye hisa nyingi.

Aliyekuwa Mkurugenzi wa Jiji la Dar es Salaam, Spora Liana (kwa sasa Mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni), mwaka 2018 alisema jiji bado ni mwanahisa, jengo na kiwanja ni mali yao, na wanahisa ni Hazina na Jiji.

**LENGO LA KARIAKOO**

Lilikuwa kiwe kituo kikubwa cha ukusanyaji bidhaa zote kabla ya kusambazwa kwenda kwenye masoko mengine, ambalo lilififia baada ya kuanzishwa Manispaa za Ilala, Ubungo, Kinondoni, Temeke, Kigamboni na Kibamba.

**ZAMANI NA SASA**

Mwonekano wake wa kipekee, ujenzi na upatikanaji wa bidhaa za kila aina, yalikuwa ni baadhi ya mambo yaliyoifanya Kariakoo iwe ya kipekee na eneo maalum ambalo wageni wengi walitamani kufika.

Shirika la Masoko Kariakoo lilianzishwa kwa ajili ya kusimamia na kuendesha masoko ya mazao ya chakula, zana za kilimo na pembejeo za kilimo jijini Dar es Salaam.

Kariakoo ya zamani ilikuwa ni magari yaliyosheheni kila aina ya bidhaa, viwe viazi ulaya, mihogo, magimbi, kabeji, vitunguu na kila aina ya chakula yalionekana yakiingia sokoni hapo kupitia mlango mkuu ulioko mtaa wa Nyamwezi yakitokomea shimoni kupakua bidhaa.

Shimoni ilikuwa ni heka heka za wabeba mizigo waliojitwisha magunia ya bidhaa kupeleka kwa wafanyabiashara ndogo ndogo, ambao walikuwa na vizimba maalum vya chuma vilivyopakwa rangi nyeupe vilivyopangwa kwenye sakafu nje ya jengo hilo kwa mpangilio maalum.

Eneo la juu lilikuwa la kuhifadhia samaki na kuuza zana za kilimo na pembejeo.

Biashara katika soko hilo ilikuwa kwa saa 24, magari ya wauzaji wa jumla huingia saa sita usiku na kuendelea, biashara huanza muda huo hadi saa 11 alfajiri ambako wanunuzi wa jumla huondoa mizigo kwenda kwenye masoko madogo na magenge yaliyoko sehemu mbalimbali za jiji, hii ndiyo ilikuwa Kariakoo ya miaka ya 70 hadi 2000.

Kariakoo ya leo, mambo ni tofauti, ukizunguka jengo la soko zimejengwa fremu za maduka ya nguo na bidhaa nyingine, huku eneo la juu ikiwa na ofisi, benki na biashara ya pembejeo.



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akikagua hatua zinazoendelea kuchukuliwa kudhibiti moto uliotokea juzi kwenye Soko la Kimataifa la Kariakoo. **PICHA: OFISI YA WAZIRI MKUU**


**JAMUHURI YA JMUUNGANO WA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA WILAYA YA KAHAMA**
**WILAYA YA KAHAMA**

**CIVIL CASE NO. 86 YA 202020**
**ALISSAR COMPANY LTD**
**........................................................MDAI**
**MDAI**
**YOHANA JUMA**
**NYANTIMB..................................................MDAIWA**
**KUITWA SHAURINI**
**KWA : YOHANA JUMA NYANTIMBA**

**POPOTE ULIPO**

Kwa kuwa mdai ameleta madai yake hapa mahakama ya wilaya kahama katika shauri tajwa hapo juu, ambalo litatajwa tarehe **15/07/2021**
Unaamriwa kuhudhuria mbele ya mahakama hii mnamo tarehe **15/07/2021 saa 2:30** asubuhi bila kukosa au kuchelewa siku hiyo ni siku ya kutajwa kwa shauri hilo ni lazima kuleta utetezi wako na Hati zote zinazohusu shauri hilo ili kujibu maombi katika shauri hilo.
Fahamu kuwa usipohudhuria siku hiyo shauri laweza kuendelea kusikilizwa na kutolewa hukumu upande mmoja bila wewe kuwepo.
Imetolwa kwa **AMRI** yangu **CHAPA** ya Mahakama hii leo tarehe 05 mwezi Julai mwaka 2021

**C.L. Chovenye**
**HAKIMU MKAZI WILAYA**
**KAHAMA**

C.L. Chovenye



**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**
**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO YA WILAYA YA NJOMBE**
**KITUO CHA NJOMBE MJINI**
**MKOA NJOMBE**
**USIMAMIZI WA MIRATHI NA 11/2021**
**VINCENT OSWARD MAJILI.........MAREHEMU**
**FATMA HASSAN NAMAGONO.........MSIMAMIZI**
**TAARIFA KWA UMMA**
**MAOMBI YA KUTANGAZA KUFUNGA MIRATHI.**

Kwa wote wanaodai kuwa na haki na marehemu aliyetajwa hapo juu wanafahamishwa kufika na kuangalia orodha ya mali za marehemu na hesabu za mirathi katika jalada la mirathi.
Mapingamizi yoyote kuhusu orodha ya mali na au hesabu za mirathi hii yawe yameandikishwa mnamo au kabla ya siku ya tarehe 30th ya mwezi wa julai mwaka 2021.

**Imetolewa na hakimu mkazi leo siku ya tarehe 05th julai mwaka 2021**

**HAKIMU MKAZI**



**KUPOTEA KWA VYETI**



**HERITUMAINIEL GERAD** anatangaza kupotelewa na vyeti vifuatavyo,cha kidato cha nne chenye index namba S 0772/0102 kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary ya **ISEVYA mwaka 2011** na cheti cha chuo cha **ST.JOSEPH UNIVERSITY** chenye namba registration namba **135104028** kozi ya **DIPLOMA IN ELECTRONICS AND COMMUNICATION ENGINEERING** mwaka 2016,yeyote atakaviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi
Polisi taarifa **RB DOD/DOD RB/341442/2021**



**KUPOTEA KWA CHETI**



116353002

**MACADAM S. MACHILU** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0335/0052** kilichotolewa na Baraza la Mitihani la Taifa kupitia MZIZIMA SEKONDARI mwaka 2007. Yeyote atakayekiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/CEN/RB/323012/2021.**



**TANZANIA AGRICULTURAL SOCIETY**
**TASO TAIFA-DODOMA**
S.L.P 1118 DODOMA

**TANGAZO TANGAZO**

KATIBU MTENDAJI WA TAASISI YA KILIMO TANZANIA AGRICULTURAL SOCIETY(TASO) ANAWATANGAZIA WANACHAMA WOTE KUWA KUTAKUWA MA MKUTANO MKUU WA TAIFA UTAKAOFANYIKA TAREHE 7/8/2021 DODOMA/MOROGORO.

TANGAZO HILI LIMEZINGATIA MATAKWA TA KATIBA YA TASO YA 1993 TOLEO LA 2009 IBARA YA 28A.

WAJUMBE WA MKUTANO HUU NI WALE WALIOTAJWA KWENYE KATIBA YA TASO YA 1993 TOLEO LA 2009 IBARA YA 9A.

UPATAPO TANGAZO HILI UNAOMBWA UMJULISHE MJUMBE WA MKUTANO HUO.

AHSANTE, PAMOJA TUIJENGE TASO

LIMETOLEWA NA:
**DASTAN B. LUKOSI**
**KATIBU MTENDAJI**

116353602

# Askofu Malasusa: Msipende umaarufu kupitia misaada

**Na Elizabeth Zaya**

ASKOFU wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Mashariki na Pwani (DMP), Dk. Alex Malasusa, amekea baadhi ya Wakristo nchini wanaotumia njia ya kuwasaidia wahitaji ili kujipatia umaarufu au kukubalika zaidi katika jamii.

Alisema kutenda matendo mema na kuyatumia kama njia ya kujitafutia umaarufu au kukubalika zaidi mbele ya jamii ni jambo ambalo halikubaliki mbele ya Mungu.

Dk. Malasusa alitoa kauli hiyo jana wakati akizindua harambee ya kuchangia ujenzi wa Chuo cha Ufundi kwa wenye ulemavu wa akili kwa vituo vya Udiakonia vilivyopo Mtoni Mtongani, uzinduzi uliofanyika katika Usharika wa Boko, Kinondoni, Dar es Salaam.

Alisema ipo tabia kwa baadhi ya watu makanisani ambao hupitia kusaidia wenye uhitaji ili wajulikane zaidi kwenye jamii.

"Wakristo wanahitaji kutenda matendo mema na siyo kuyatumia kama kitu cha kuwafanya wajulikane zaidi au kukubalika katika jamii, wapo wachache makanisani ambao wakitoa wanataka wajulikane," alisema Dk. Malasusa.

"Mtumikieni Mungu kwa kusaidia wahitaji na iwe kama tabia, toa au saidia na ikiwezekana hata Askofu wako asijue ila Mungu tu ndiye ajue, na watu wa namna hii wanaopenda kujulikana wanaposaidia ndiyo wale wanaoangalia sadaka kama kodi, na wanapotoa wanamuangalia mchungaji na siyo Mungu, hauwezi kusema unampenda Mungu kama husaidii wahitaji."

"Na kutenda mema siyo kwa matajiri tu ni kwa kila mtu na hii ni tabia binafsi na ndiyo maana kunapotokea harambee kama hizi watu wanaalika tu wale wenye kampuni, kumtolea Mungu au kumsaidia mwenye uhitaji hakuhitaji tajiri tu, huu ni moyo wa mtu ambaye anatoa kile alichonacho kwa ukamilifu."

Kwa upande wake, Naibu Katibu Mkuu huduma za jamii, kutoka katika kituo cha Udiakonia KKKT Mtoni Mtongani, wilayani Temeke, Agnes Lema, alisema ujenzi wa chuo hicho kwa ajili ya vijana wenye ulemavu wa akili utasaidia kuongeza nafasi za kupata elimu bora kwa watoto wenye ulemavu huo wa akili.

"Wazo la kuwa na chuo hiki cha ufundi kwa wenye ulemavu lilikuja baada ya kushuhudia vilio vya miaka mingi kutoka kwa wazazi na watoto pindi wanapomaliza muda wa kukaa kwenye kituo chetu cha Mtoni na wengine walikuwa wakikataa kuondoka," alisema Lema.



Mkuu wa Wilaya ya Bunda mkoani Mara, Joshua Nassari, akipata maelezo kutoka kwa mhudumu wa duka la Vodacom baada ya kuzindua duka hilo, wilayani humo mwishoni mwa wiki. Vodacom Tanzania Plc ilizindua duka hilo wilayani Bunda ikiwa ni juhudi za kuhakikisha wanaleta huduma bora karibu na wateja wake. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Barakoa sokoni, 'level seat' kwenye daladala lazima

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na mlipuko wa homa kali ya mapafu inayosababishwa na virusi vya corona wimbi la tatu, Mkoa wa Dodoma umewaagiza wafanyabiashara wote katika masoko, minada na maeneo yenye mikusanyiko kuvaa barakoa na atakaye kaidi hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

Aidha, umepiga marufuku wamiliki wa vyombo vya usafiri hususani daladala kupakia abiria zaidi ya idadi ya viti kuanzia leo.

Maagizo hayo yalitolewa na Mkuu wa mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alipokuwa akieleza mikakati ya mkoa huo katika kukabiliana na virusi vya corona wimbi la tatu.

Mtaka, alisema kutoka na mlipuko huo wa virusi vya corona hivi sasa nchini, mkoa wake umejipanga kikamilifu kuimarisha mikakati ya kuukabili ipasavyo.

Alisema moja kati ya mikakati ni kutoa maelekezo kwa wamiliki wa vyombo vya usafiri hasa daladala katika Jiji la Dodoma kuhakikisha kuwa wanapakia abiria kulinga na idadi ya viti (Level seat).

"Lakini pia katika masoko yote yaliyopo mkoani Dodoma tutahakikisha kuwa kunakuwapo na maji tiririka na sabuni, na kila mafanyabiashara lazima avae barakoa anapotoa huduma," alisema Mtaka. Aidha, alisema mfanyabiashara atayekaidi kuvaa barakoa hataruhusiwa kuingia ndani ya soko kufanya biashara na hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

"Hii ni pamoja na wafanyabiashara katika mnada wa Msalato na minada mingine, hatuwezi kufunga mnada huu kwa sababu ya watu wachache ambao hawataki kufuata maelekezo ya wataalamu wa afya ya kuvaa barakoa na kunawana mikono," alisema.

Vile vile, Mtaka alisema katika mnada wa Jumamosi ijayo watatuma wataalamu wa afya kwenda kufanya ukaguzi kama maelekezo hayo yametekelezwa.

Alisema mnada huo unajumuisha watu wengi kutoka katika mikoa mbalimbali hali ambayo inaweza kusababisha mlipuko wa virusi hivyo kwa haraka kama hatua za haraka hazitachukuliwa.

"Nitowe wito kwa Watanzania wenzangu tusife kizembe eti tuu kwa kukosa kuvaa barakoa ya 'buku'...endelea kunywa bia, lakini kumbuka kuvaa barakoa corona ipo na inaua na wanaokufa ni watu siyo miti," alisisitiza Mtaka.

Mtaka, alisema kuwa uhai wa mtu sio mali ya serikali hivyo ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha anajilinda kwa kuchukua tahadahari zote dhidi ya virusi vya corona.

Juzi Waziri wa Afya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, alisema kuwa wagonjwa wa homa kali ya mapafu, inayosababishwa na virusi vya corona imefikia 408, huku 284 wakitumia msaada wa mitungi ya oksjeni kupumua.

Dk. Gwajima alitoa takwimu hizo wakati alipokuwa akitoa elimu kwa jamii kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Alisema kuwa hadi kufikia Julai 8, mwaka huu wagonjwa 284, kati ya 408 wanapumua kwa kutumia mashine za oksijeni.

Alisema kwa Dodoma takwimu zinaonyesha hadi Julai 8, mwaka huu kulikuwa na wagonjwa 26, kati yao 22 wanapumua kwa msaada wa mashine.

# Baba aua mwanawe kwa panga

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

JESHI la Polisi mkoani Rukwa linamsaka, Allon Simfukwe, mkazi wa Kitongoji cha Kaloleni Manispaa ya Sumbawanga kwa tuhuma za kumuua mtoto wake Kadius Allon (3), kwa kumkata na panga.

Akizungumza na waandishi wa habari, Kamanda wa Polisi Mkoa wa Rukwa, William Mwampaghale, alisema mtuhumiwa huyo anadaiwa kumuua mtoto wake kwa kumpiga na panga, kwamba tukio hilo lilitokea Julai mosi, mwaka huu katika Kitongoji cha Kaloleni.

Alisema Jeshi la Polisi linaendelea kumtafuta ili achukuliwe hatua za kisheria.

Inaelezwa kwamba licha ya kudaiwa kutekeleza tukio hilo, Simfukwe amekuwa akitoa lugha za vitisho kwa Mwenyekiti wa Mtaa.

Inadaiwa kuwa kabla ya Simfukwe kufanya mauaji hayo alikuwa na mgogoro wa kifamilia na mkewe uliosababisha mwanamke huyo kukimbilia nyumbani kwao na kumuacha mtoto huyo akiwa na baba yake.

Kadhalika, inaelezwa kuwa Simfukwe aliendа ukweni na kufanya fujo, ikiwamo kumkata panga mama mkwe kwa madai kwamba amekuwa akikumbatia uovu wa mtoto wake.

Kamanda Mwampaghale alisema licha ya tukio hilo kuripotiwa polisi, wanandugu walingilia kati na kumaliza mgogoro kimya kimya, Simfukwe alimtaka mkewe kurudi nyumbani ili wasaidiane kulea mtoto.

Kamanda Mwampaghale alisema mwanamke huyo hakuwa tayari kurudi kwa mumewe kutokana na kipigo anachopata mara kwa mara.

Kamanda Mwampanhale alisema Julai mosi, Simfukwe alifika nyumbani kwa wakwe nyakati za usiku na kuomba kufunguliwa mlango kwa lengo la kutaka kuzungumza na mke wake, kitendo ambacho hakikufanyika.

Alisema baada ya kuzuiliwa kuzungumza na mke wake, Simfukwe alieleza kwamba atamuua mtoto, kitendo ambacho anadaiwa kukitekeleza kisha kumtupa mtoto uani mwa nyumba hiyo.

Kamanda Mwampaghale alisema baada ya muda mama mkwe wake na mkewe walipoenda uani mwa nyumba hiyo walimkuta mtoto huyo akiwa na majeraha ya kukatwa na panga, hivyo walimchukua mtoto huyo na kumkimbiza hospitali ambako alifariki dunia muda mfupi baadaye.

Kamanda Mwampaghale alisema licha ya kudaiwa kutekeleza kitendo hicho, Simfukwe pia aliandika ujumbe katika karatasi na kuutupa maeneo ya karibu na kituo kikuu cha polisi mjini Sumbawanga unaosema: "Kwa kuwa mke wangu amegoma kurudiana na mimi nakwenda kujinyonga."

HABARI KITAIFA

# Talaka chanzo utoro shuleni Nanyumbu

**Na Hamisi Nasri,** NANYUMBU

TALAKA holela na kilimo cha kuhamahama wilayani Nanyumbu mkoani Mtwara, zimetajwa kuwa ni chanzo cha utoro katika shule za msingi.

Imeelezwa wastani wa wanafunzi 100 hutoroka kila siku wa shule za msingi Likokona 'B' na Mangaka.

Hayo yalibainishwa jana na wadau wa elimu wilayani Nanyumbu waliokutana kujadili taarifa ya zoezi la ufuatiliaji katika sekta ya elimu iliyotolewa na Mtandao wa Mashirika yasiyo ya Kiserikali mkoani Mtwara, (Mtwangonet) kwa kushirikiana na Asasi ya Wajibu.

Akisoma taarifa ya ufuatiliaji sekta ya elimu, Mratibu wa Mtwangonet, Fidea Ruanda, alisema hivi karibuni walifuatilia hali ya elimu kwenye sekta ya elimu wilayani humo na kubaini changamoto nyingi.

Alizitaja ni utoro wa wanafunzi ambao unasababishwa na sababu nyingi, ikiwamo ya kuvunjika kwa ndoa kiholela, watoto kutopata chakula, umaskini wa familia na hali duni ya miundombinu.

Ruanda alisema ufuatiliaji walioufanya katika Shule ya Msingi Likokona 'B' na baadhi ya shule zingine walibaini wanafunzi zaidi ya 100 kwa siku hawahudhurii shuleni kwa sababu ya matatizo mbalimbali ikiwamo migogoro ya ndoa.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Msingi Likokona 'B', Faraji Namulichi, alisema katika shule yake kuna tatizo kubwa la utoro wa wanafunzi na alipofuatilia alibaini wengi huishi na mzazi mmoja baada ya wazazi kutalikiana.

Alisema kuna haja ya kushirikiana kati ya kamati za shule, serikali na jamii kuhakikisha suala la utoro shuleni linakomeshwa ikiwa ni pamoja na kuweka sheria ndogo za kudhibiti utoro.




Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Ummy Mwalimu (katikati), akikagua vifaa tiba vilivyotolewa na Benki ya Maendeleo (TIB) kwa ajili ya Hospitali ya Wilaya ya Kasulu, mkoani Kigoma. Kulia ni Naibu Katibu Mkuu TAMISEMI (anayeshughulikia afya), Dk. Grace Magembe na kushoto ni Meneja Masoko na Uhusiano wa Benki ya Maendeleo TIB, Saidi Mkabakuli. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mwinyi acharuka ataka uchunguzi wizi fedha za umeme

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, ameziagiza Taasisi ya Kupambana Rushwa na Uhujumu Uchumi Zanzibar (ZAECA) pamoja na Jeshi la Polisi kuchunguza suala la wizi wa Fedha za Shirika la Umeme (ZECO) katika vituo vya shirika hilo, huku akitaka hatua za kisheria zichukuliwe kwa watakaobainika kuhusika na kadhia hiyo.

Aliyasema hayo wakati akizungumza na watendaji mbalimbali wa serikali katika majumuisho ya ziara yake Mkoa wa Mjini Magharib Unguja juzi.

Alisema kuna wizi mkubwa wa fedha katika vituo vya kuuzia umeme na kuzitaka taasisi hizo kufanya uchunguzi wa kadhia hiyo na atakayegundulika kuchukuliwa hatua za kisheria.

Pia aliagiza kusimamishwa kazi wafanyakazi waliohusika na ung'oaji wa nguzo za umeme katika eneo la Mwachealale, Wilaya ya Magharib A Unguja.

Rais Dk. Mwinyi aliikumbusha ZECO kuwa ni wajibu wake wa kupeleka nguzo za umeme pamoja transfoma katika shughuli za kuwaungia umeme wananchi.

"ZECO wana wajibu wa kupeleka nguzo za umeme na transfoma, suala la ada nalo litazamwe upya," alisema.

Akigusia sekta ya ujasiriamali, Dk. Mwinyi aliagiza mifuko yote ya uwekezaji iliyopo nchini, iunganishwe (ukiwamo Mfuko wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi, Mfuko wa wenye ulemavu, Vijana, SMIDA n.k), kwa kuwa haijafanya kazi ipasavyo, kutokana na fedha kutolewa ovyo na bila hesabu, pamoja na kutokuwapo marejesho.

Aidha, ameitaka Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi kuwawezesha wajasiriamali, huku akitaka fedha zitumike vizuri, na kutoa mfano wa matumizi mabaya ya fedha kwa SMIDA, ambao katika kipindi cha mwaka mzima iliwawezesha wananchi 27 pekee kupata mtaji wa Sh. bilioni mbili.

Katika hatua nyingine, Rais Mwinyi, amezungumzia suala la usafi katika Jiji la Zanzibar, na kusema ni eneo la barabara ya Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Abeid Amani Karume kuelekea Hospitali ya Rufani ya Mnazi mmoja pekee, ndiyo inayosafishwa kwa kuwa anaitumia kuelekea Ikulu.

"Hakuna eneo lolote lililo safi zaidi ya ile ya Airport ambayo inasafishwa kwa vile mimi napita," alisema.

Alisema asilimia 90 ya fedha za mradi wa ZUSP ambazo ni Dola za Marekani milioni 90, zimetengwa kwa ajili ya kupendezesha mji, lakini hakuna matunzo ya miti iliyopandwa, mbali na fedha nyingi kutumika kwa ajili kuilipa kampuni ya usafi.

Alisema serikali inakusudia kuja na mradi maalum wa kupendezesha mji kwa kuwa na barabara zenye lami, maeneo ya waenda kwa miguu pamoja na mambo mbalimbali, huku jukumu la kusimamia usafi likiwa chini ya usimamizi wa manispaa.

Vile vile, alisema hadi sasa hakuna hatua zozote zilizochukuliwa za ujenzi wa masoko au vituo vya mabasi na manispaa imejikita katika mikataba ya ovyo.

Kuhusu Sekta ya Ardhi na Makazi, Dk. Mwinyi alisema kumekuwapo na migogoro mbalimbali katika maeneo aliyoyatembelea, na Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makazi imejikita katika utatuzi wa migogoro, badala ya kuja na mipango mipya ya maendeleo.

Aliahidi kuunda tume itakayokuwa na wajibu wa kupitia migogoro yote ya ardhi na wizara kubaki na jukumu la kuendeleza makazi mapya kwa wananchi.

Pia, watendaji wote watakaobainika kuhusika au kuwa chanzo cha migogoro hiyo, tume itakayoundwa itawachukuliwa hatua.

Akizungumzia udhalilishaji wa kijinsia pamoja na upatikanaji wa dawa la kulevya, alizitupia lawama mamlaka zinazohusika kwa kutokuchukua hatua zozote za msingi katika kukabiliana na jambo hilo.

Alivitaka vyombo vya ulinzi na usalama pamoja na wadau kushirikiana kuondoa udhalilishaji nchini na kuagiza watuhumiwa wote wa makosa hayo kuwekwa ndani.

Alisema vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia dhidi ya wanawake na watoto unaanzia kwenye jamii (shule, madrasa), na kuitaka jamii kuondokana na muhali.

Akigusia dawa za kulevya, alisema mihadarati hiyo imekuwa ikiingia nchini kupitia njia za bandari na uwanja wa ndege na kubainisha uwapo wa baadhi ya watendaji wanaoshirikiana na wahalifu kupitisha dawa hizo na kuleta athari kubwa kwa vijana na wengi wao hujiingiza katika vitendo vya wizi.

# Wachimbaji wadaiwa kutorosha madini

**Na Mohab Dominick, KAHAMA**

BAADHI ya wachimbaji wadogo wa dhahabu katika Mgodi wa Kabela Mwime, Kata ya Zongomela wilayani Kahama mkoani Shinyanga, wamebainika kufanya utoroshaji wa mawe yanayosadikiwa kuwa na dhahabu kwa kushirikiana na viongozi wa mgodi huo.

Mawe hayo hutoroshwa na wachimbaji wa eneo hilo nyakati za usiku kati ya kuanzia majira ya saa tisa mpaka saa 11 alfajiri na kuwauzia wafanyabiashara wa eneo hilo jambo ambalo ni kuihujumu serikali.

Hayo yalielezwa juzi na Mkaguzi wa Madini wa Tume ya Madini Mkoa wa Kimadini Kahama, Deogratius Subaila, wakati akizungumza kwenye mkutano uliolenga kutoa elimu kwa wachimbaji wadogo wa Mwime uliohusisha wachimbaji hao wa dhahabu na maofisa wa madini kilichofanyika kwenye viwanja vya ofisi za mgodi wa Kabela.

Alisema kuna watu wanatorosha mawe yanayosadikiwa kuwa na dhahabu nyakati za usiku kuanzia saa tisa mpaka saa 11 alfajili na mawe mazuri yenye dhahabu hupembuliwa na kuachwa duarani ambapo ukifika wakati watu wamepungua mitaani walinzi wa mgodi huyasomba na kwenda kuyauza.

Kutokana na hali hiyo, Ofisi ya Madini Mkoa wa Kimadini Kahama imebaini uwapo wa wimbi kubwa la wizi wa mawe yanayosadikiwa kuwa na dhahabu kwenye mgodi huo wa Kabela.

Aidha, alisema mawe hayo yanatoroshwa kupitia soksi za kuvaa miguuni, mifuko midogo midogo inayovaliwa na koti kubwa.

"Ofisi ya mgodi wa Kabela inahusika, walinzi wanaolinda nyakati za usiku ndiyo wanaoendesha zoezi la wizi wa mawe, ambayo yanasotiwa na kuachwa chini ya duara lakini yanatolewa nyakati za usiku, na wanaoyatoa ni wachimbaji ambao ni wanachama kwenye kikundi cha mgodi naomba muache mara moja tabia hii," alionya Subaila.

Naye Ofisa Madini Mkazi wa Mkoa wa Kimadini Kahama, Mhandisi Joseph Kumburu, alidhibitisha uwapo wa matukio hayo na kuwataka wachimbaji wa Mwime kutotetea wezi badala yake waonyeshe ushirikiano kwa Ofisi ya Tume ya Madini Kahama ili kupunguza wimbi la utoroshwaji wa mawe.

Mpaka sasa watu 30 wanaojihusisha na ununuzi wa mawe ya dhahabu huko Kakola Kata ya Bulyanhulu na Kata Segese wanashikiliwa na Polisi, jambo ambalo limeifanya Tume ya Madini kurudi migodini kutoa elimu kwa wachimbaji hao ili kuepuka utoroshaji wa dhahabu.

Katibu wa Mgodi wa Kabela, Jomanga Mzee alikana ofisi ya mgodi kuhusika badala yake alisema waliofanya wizi huo ni watu wanaoitwa 'manyani' wanashirikiana na wanachama wa maduara kufanya hivyo.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Poleni Polisi, ni wakati klabu kuungana

**TASNIA** ya michezo nchini imepokea kwa mshtuko habari za ajali ya timu ya mpira wa miguu ya Polisi Tanzania siku ya Ijumaa.

Kwa mujibu wa Kamanda wa Polisi mkoani Kilimanjaro, Simon Maigwa ni kwamba ajali hiyo ya wachezaji wa Polisi Tanzania ilitokea saa tano asubuhi maeneo ya TPC Moshi wakitoka mazoezini.

Basi walilopanda likiwa na wachezaji 32, makocha na madaktari liligonga mti na kuacha njia, likisababisha wachezaji 16 kujeruhiwa, huku straika tegemeo wa klabu hiyo, Gerald Mdamu akivunjika miguu yote miwili.

Polisi Tanzania walikumbwa na janga hilo wakitokea mazoezi kujiandaa na mechi dhidi ya Kagera Sugar iliyotarajia kuchezwa Julai 14.

Nipashe linatoa pole kwa wachezaji, viongozi, benchi la ufundi, madaktari, ndugu na jamaa walioguswa na janga hilo, pamoja na Jeshi la Polisi kwa ujumla.

Tunaomba kwa Mungu awajalie wote waliopatwa na ajali afya njema, wapate nafuu, na hatimaye kupona, ili kurejea kwenye majukumu yao ya kawaida ya kazi zao.

Uzuri ni kwamba karibuni klabu zote za Ligi Kuu zimetuma salamu za pole na kuwatakia wapone haraka.

Klabu za Ligi Kuu na Daraja la Kwanza, Shirikisho la Soka na Bodi ya Ligi, zote zimeungana pamoja, zikionyesha kusikitishwa na wenzao kupatwa na janga hilo.

Hili limeonyesha upendo wa hali ya juu ambao haukudhaniwa kuwepo kwenye tasnia hiyo.

Wengi walidhani soka ni kama vita, kazi yao ni kupambana tu uwanjani na upinzani unabaki hivyo hivyo hata baada ya mechi kumalizika.

Nipashe tunaona kwamba, ajali hiyo imeonyesha umoja wa klabu zote za Tanzania. Zimeonyesha kuwa upinzani wao ni dakika 90 tu, lakini baada ya hapo wanabaki kuwa ni jamii ya soka na wote ni ndugu.

Tunaupongeza sana umoja huu ulioonyeshwa na klabu za Ligi Kuu na tunaamini hautaishia hapo.

Inawezekana umoja huu ukawa chachu ya kuundwa kitu ambacho kitazisaidia klabu na wachezaji kwa ujumla.

Ikumbukwe kuwa wachezaji wa klabu hizi wako kwenye mazingira ya hatari muda wote, wawapo ndani ya nje ya uwanja.

Wanachezaji wana mchezo wa hatari ambao unaweza kuwafanya wawe walemavu. Pia karibuni mwaka mzima wanasafiri, iwe kwenye ndege au gari.


Hivi vyote ni vyombo vya moto ambavyo havina dhamana kama tulivyoona kwenye ajali ya Polisi Tanzania.

Mfano ni mchezaji Gerald Mdami kwa sasa amevunjika miguu yote miwili. Bila kupindisha maneno ni kwamba anahitaji muda mrefu wa kukaa kabla ya kurejea tena uwanjani. Lakini anatakiwa yeye na familia yake waishi na kupata mahitaji.

Nipashe tunashauri kuwa ajali hii ya Polisi Tanzania na umoja huu ulioonyeshwa na klabu, utengeneze kitu ambacho kiwe kama mfuko wa maafa kwa ajili ya wachezaji, viongozi, benchi la ufundi, Maofisa Habari na hata madaktari waoambatana na timu ili kuweza kuwasaidia wanapopatwa na matatizo kama hayo.

Klabu zitengeneze utaratibu wa kukata asilimia fulani za pesa za viingilio ziingie kwenye mfuko huo kwa ajili ya kuwasaidia waathirika.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Sifa za Mauya zinapoenda kwa mzee Mpili

Na Adam Fungamwango

**DAKIKA** ya 11, Zawadi Mauya anaukuta mpira uliokuwa unazagaazagaa kwenye eneo la hatari la timu ya Simba. Anaachia shuti kali linalombabua Shomari Kapombe na kujaa wavuni.

Linakuwa ni bao pekee la Yanga kwenye mechi ya watani wa jadi ya mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara iliyochezwa kwenye Uwanja wa Benjamin Mkapa, Julai 3, mwaka huu.

Yanga iliondoka na ushindi wa bao 1-0 kwenye mechi ambayo si wengi waliootarajia kuwa wangeweza kuibuka na ushindi.

Ni mechi ambayo Kocha Mkuu wa Yanga, Nasreddine Nabi aliifanya timu yake kucheza kwa mbinu zaidi ili kuikabili Simba, timu ambayo kama ukiingia kichwa kichwa inakumaliza.

Baada ya mechi hiyo kumalizika kulitokea kitu cha acha ajabu. Sifa za ushindi wa Yanga zikahamia kwa mzee mmoja anaitwa mzee Mpili.

Ni mzee ambaye kabla ya mechi hiyo alijichukulia umaarufu wa muda kwa kuwananga baadhi ya viongozi wa Yanga, lakini akiwatahadharisha kutopeleka timu uwanjani kwenye mechi hiyo ya Julai 3, kama ilivyokuwa mwanzo Mei 8.

Hata hivyo, viongozi wa Yanga walikuwa makini. Walisimamia msimamo wao wa kupeleka timu.

Mwishoni akaungana na wenzake kuwa watapeleka timu na kudai kuwa watashinda.

Na kweli timu ikashinda. Sifa zote zikaelekezwa kwake. Ukiwasiliza wote wanaommiminia sifa mzee Mpili, hawana hoja zaidi ya imani za kishirikina.

Mambo ya dhana za ushirikina kwenye klabu za Simba na Yanga na hasa kwenye mechi zao zipo tangu enzi na enzi. Lakini huwezi kuzikuta kwenye vyombo vya habari. Na hasa redio na baadhi ya magazeti, hasa ya michezo.

Kwenye dunia ya sasa ya sayansi ya teknolojia, hasa mitandao ya kijamii, nilitegemea zaidi sifa za mzee Mpili zingekuwa kwenye mitandao ya kijamii zaidi kuliko redio na magazeti.

Ingekuwa kwenye mitandao ya kijamii na baadhi ya 'blogu' wala nisingeshangaa kwa sababu mara nyingi hutumika wakati mwingine kuwafanya watu wafurahi, wacheke na kushangazwa kwa taarifa kama hizo.

Lakini utashangaa baadhi ya vipindi vya michezo, wenye watangazaji na wachambuzi wabobevu kuacha kuzungumzia mechi jinsi ilivyokuwa. Ufundi wa mchezaji mmoja mmoja na jinsi gani Yanga walivyocheza hadi kupata ushindi, badala yake kumpa sifa zaidi mzee Mpili.

Hii ina maana wachambuzi wameacha kazi yao ya kuchambua mpira na sasa wanazungumzia vitu ambavyo hawana uhakika navyo na wala havichambuliki.

Hata alipoitwa kwenye baadhi ya vyombo vya habari, mzee Mpili alishindwa kuweka wazi, au kuchambua ni jinsi gani alivyofanya hadi Yanga kupata ushindi. Alichukua nini na kipi na kukiweka wapi hadi Yanga ikashinda?

Hata Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Fredrick Mwakalebela, alionekana kushangazwa ni kwa nini baadhi ya redio, televisheni na baadhi ya magazeti wamempa nafasi sana mzee huyo zaidi ya mfungaji mwenyewe wa goli, Zawadi Mauya.

Ni kweli kabisa alivyosema Mwakalebela, kwani baadhi ya mashabiki wa Yanga hata mfungaji wa bao hawamjui, lakini wanamfahamu mzee Mpili, mtu ambaye ameipa Yanga ushindi dhidi ya Simba kwa mbinu za kufikirika.

Mimi nadhani watu wa habari wangejikita zaidi kwenye mambo ambayo yanazungumzika na kuchambulika, kuliko kushabikia zaidi dhana, hasa za ushirikina.

Kumkumbatia mzee Mpili na kumfanya mada ni kufundisha watu au vijana kuwa kwenye mpira kuna mambo ya kishirikina ambayo yanaweza kuifanya timu ikapata ushindi.

Hii itawapotosha vijana wengi ambao tumeanza kuwaaminisha kuwa kuwekeza pesa, kuwa na wachezaji wazuri, mazoezi, na kujituma ndiyo njia pekee ya timu kupata ushindi na mafanikio ya klabu.

Badala ya timu sasa kuwekeza huko, ukakuta vijana wetu sasa wakaanza kuwatafuta kina mzee Mpili wengine ili wapate ushindi.

Ushindi huu wa Yanga si wachezaji wala kocha Nabi ambaye wameufaidi kwa kuwamwagiwa sifa. Wote wamefichwa kwenye kivuli cha mzee Mpili, hivyo kuwafanya hata baadhi ya watu ambao wao ni wafuata mkumbo tu kuamini kuwa bila mzee huyo isingeshinda.

Ifikie wakati sasa watangazaji wa wachambuzi waendelee kujikita zaidi na kuchambua soka kiufundi, timu ikishinda iangaliwe ilishinda kwa sababu gani na hata ikifungwa ielezwe ni sababu gani ilisababisha ipoteze na hata sifa zielekezwe kwa walioifanya kazi hiyo.

Mambo mengine hasa ya nje ya uwanja hasa yenye mlengo wa kishirikina, wayaache kwenye mitandao ya kijamii ili iwe burudani na 'mazungumzo baada ya habari' vijiweni.

# Kimbiji waondokana kero ya maji

**Na Joseph Mwendapole**

WAKAZI wa Kijiji cha Kizito Wonjwa, kilichopo Kimbiji Kigamboni Dar es Salaam, wameondokana na kero ya maji ya muda mrefu baada ya kukabidhiwa kisima cha maji kinachotumia nishati ya jua kusukuma.

Kisima hicho kilichokabidhiwa mwishoni mwa wiki na Kampuni ya Davis & Shirtliff (D&S) Group, inayojihusisha na usambazaji na uuzaji wa vifaa vya maji nchini Tanzania kimegharimu Sh. milioni saba.

Akizungumza wakati wa hafla ya kukabidhi kisima hicho, iliyofanyika katika kijiji cha Kizito Wonjwa, mwishoni mwa wiki, Mkurugenzi wa D&S, Benjamin Munyao, alisema mashine iliyowekwa inawasaidia wakazi hao kuchota maji bila kutumia mikono yao kusukuma bomba.

"Mtambo huu unaotumia nishati ya jua una uwezo wa kusukuma lita 500 hadi 1000 za maji kwa saa. Mfumo wa nishati ya jua pia unarahisisha kituo hicho kufanya kazi kwa saa 24," alisema.

Alisema kisima hicho ni ukombozi kwa wakazi wa kata ya Kimbiji ambao walikuwa wakitegemea visima vifupi ambavyo hukauka maji mara kwa mara.

Mkazi wa kijiji hicho, Sanata Omary (30), alisema kabla ya msaada huo alikuwa akiamka saa 10 usiku na kuiacha familia yake ikiwa imelala kwenda kuchota maji na hata hivyo wakati mwingine alikuwa akiyakosa.

"Kuoga ilikuwa ni jambo kama la anasa sana kwetu. Watoto walilazimika kuosha uso tu kabla ya kwenda shule na wakati wa kulala ilinibidi nitafute maji wakati wa usiku mwingi, lakini kwa sasa ana kila sababu ya kutabasamu kwa sababu D&S wamewezesha upatikanaji wa majisafi na salama ambayo yanakidhi mahitaji," alisema.

Alisema baada ya msaada huo yeye na familia yake wanajisikia salama kupata maji wakati wowote na anatumia muda mwingi kufanya shughuli zingine za maendeleo pamoja kuitunza familia yake.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Kigamboni, Ofisa Tarafa wa Pemba Mnazi, Bwana Msigwa, aliahidi kutunza miundombinu hiyo ya maji na kuomba wadau hao wa maendeleo kuendelea kujenga visima na mabomba ya kisasa katika maeneo mengine yenye changamoto. "Hivi karibuni, kumekuwa na wimbi la wizi wa sola kwenye hii tarafa kwasababu zaidi ya sola sita zimeibiwa ndani ya miezi miwili. Sasa ninatangaza msako mkali wa wezi hao ili kuhakikisha miundombinu ya maji kama hii inalindwa na kuwanufaisha wananchi wote," alisema.




Ofisa Mkuu wa Wateja Binafsi na Biashara, Filbert Mponzi (kushoto) na Mkuu wa Kitengo cha Bidhaa, Aloyce Maro (kulia), wakizindua bidhaa mpya ya Benki ya NMB 'SPEND 2 SAVE', mteja aliyejiunga atanufaika na faida kadri anavyofanya matumizi yake. Wengine katikati wakishuhudia ni maofisa waandamizi wa benki hiyo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wamlilia Samia nyumba zao 100 kubomolewa

**Na Richard Makore,** TARIME

WANANCHI wanaomiliki nyumba zaidi ya 100 zenye hati miliki ikiwamo ya aliyewahi kuwa Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi, Hayati Jenerali Mwita Kyaro, wamemwangukia Rais Samia Suluhu Hassan kuwanusuru wasivunjiwe bila fidia ili kupisha ujenzi wa barabara.

Wakala wa Barabara (TANROADS), umetoa notisi ya siku 30 mpaka mwisho wa mwezi huu, wananchi hao wawe wamebomoa nyumba zao na kupisha ujenzi wa barabara ya Tarime hadi Natta wilayani Serengeti mkoani Mara yenye urefu wa kilomita 87.

Kwa mujibu wa notisi iliyotolewa na Meneja wa TANROADS Mkoa wa Mara, Mrimi Ngaire, wananchi hao wasipovunja nyumba zao wenyewe watalazimika kulipa serikali gharama za kuvunja.

Wakizungumza na waandishi wa habari wilayani Tarime mwishoni mwa wiki, walisema mtu pekee kwa sasa anaweza kuwasaidia ni Rais Samia kwa kuwa wanaona wanaonewa.

Walisema wamejaribu kutumia njia zote za kutafuta haki, lakini wanaona wanaelekea kushindwa na kumuomba Rais Samia atumie mamlaka yake ili kama wanabomolewa basi walipwe fidia kwa sababu wanamiliki maeneo hayo kihalali kwa hati zilizotolewa na serikali.

Kwa mujibu wa wananchi hao, walipewa viwanja hivyo na serikali miaka ya 70 na kupewa hati halali zilizotolewa na kamishna wa ardhi, lakini wanashangaa kupewa siku 30 ili wavunje nyumba zao.

Katika kikao kilichofanyika mwishoni mwa wiki mjini Tarime kati ya TANROADS, Naibu Waziri wa Ujenzi na Uchukuzi, Mwita Waitara na wananchi hao, waliambiwa kwamba lazima wabomoe nyumba zao bila kulipwa fidia.

Kabla ya kutolewa msimamo huo wa serikali, wananchi hao walipewa nafasi ya kuzungumza na kuonyesha vielelezo vyote vya umiliki wa nyumba hizo kihalali.

Akitoa msimamo wa serikali, Ngaire alisema, wameishatangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa barabara hiyo na kuwataka wananchi hao kuanza kubomoa nyumba zao.

Licha ya wananchi hao kuonyesha hati za kumiliki ardhi hiyo, Ngaire alisema wakala haujui suala hilo na kama serikali ilifanya makosa huko nyuma wao hawana namna ya kufanya.

"Kama kuna makosa yalifanywa na serikali huko nyuma kwa kutoa hati katika eneo la barabara, sisi hatujui hilo mnachotakiwa ni kubomoa nyumba zenu ili mradi uanze kutekelezwa," alisema Ngaire.

Alisema nyumba hizo zinatakiwa kuwa umbali wa mita 22.5 kila upande wa barabara, huku wananchi wakisema zamani wkati wanapewa hati waliambiwa ni mita 21.5 kwa kila upande.

Wananchi hao walikata tamaa baada ya Waitara kupigilia msumari wa mwisho kwamba, lazima watu hao wabomoe nyumba zao na kuondoka kupisha ujenzi wa barabara.

Alisema barabara hiyo ni muhimu kwa ajili ya kufungua uchumi wa Wilaya ya Tarime na maeneo mengine ya jirani ikiwamo nchi jirani ya Kenya pamoja na hifadhi ya mbuza ya Serengeti.

"Leo nimekuja kuwaeleza kwamba hii barabara lazima ijengwe kutoka hapa hadi Serengeti kwa takribani kilomita 87... na hii barabara tuliomba fedha bungeni na tukapewa za kujenga kilomita 25 katika awamu ya kwanza, watatushangaa tukishindwa kuijengwa kwa kuwa una nyumba za watu," alisema Waitara.

Aliongeza kuwa anajua wananchi hao wanamiliki maeneo yao kihalali kwa kuwa walipewa hati, lakini suala la barabara na lenyewe lina umuhimu wake wa kipekee.

# Bandari ilivyopaisha mapato kwa miezi 3

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) imesema katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Aprili hadi Juni mwaka huu kumekuwa na ongezeko kubwa la mapato ambayo yamepanda hadi kufikia Sh.bilioni 236 kutoka Sh.bilioni 203 katika kipindi kama hicho mwaka jana.

Pia, imesema kwa kipindi cha Mei pekee mwaka huu, Mamlaka hiyo ilifikisha mapato ya Sh. bilioni 84, na kwamba kiwango hicho kwa mwezi kama huo hakijawahi kufikiwa kwa miaka mitano iliyopita.

Kauli hiyo ilitolewa na Meneja Uhusiano na Mawasiliano wa TPA, Nikodemus Mushi, kwenye banda la Mamlaka hiyo katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam(DITF).

"Kwa hiyo kuna ongezeko kubwa la mapato na kiwango hiki tunasema ni kikubwa sana katika rekodi zetu," alisema Mushi.

Alisema sababu kubwa ambazo zimechangia kufikia kiwango hicho cha mapato ni uwekezaji mkubwa uliofanywa kwenye mitambo na teknolojia, hamasa iliyopo miongoni mwa wafanyakazi, Bodi na Menejimenti ya Mamlaka hiyo.

"Kumekuwa na mambo mbalimbali yametokea, lakini kwa sasa tuna uongozi mpya, tuna mshikamano na tunaona kero nyingi zinashughulikiwa kwa haraka, kero za ndani na nje ya taasisi, kwa hiyo zimeanza kuleta mafanikio ambayo tunayaona kupitia mapato na huduma mbalimbali," alisema Mushi.

Alitaja eneo jingine ambalo TPA imepata mafanikio makubwa katika kipindi cha miezi hiyo mitatu ni katika miradi ya upanuzi wa bandari pamoja na mitambo.

"Serikali ya awamu ya sita imetoa Sh. bilioni 96.7 na zimetolewa katika mfumo wa barua za dhamana zinazotuwezesha kuleta mitambo na kufanya kazi kwa ufanisi bandarini ... hii ni hatua kubwa kwa sababu ni kwa mara ya kwanza tunapata hizi barua kwa wakati mmoja zenye kiwango kikubwa namna hii cha pesa," alisema Mushi.

"Hizi ni barua maalum ambazo zinatolewa na serikali kama dhamana ya kuthibitisha kwamba tuna uwezo wa kulipia mitambo na vifaa mbalimbali vya kufanyia kazi, kwa hiyo tunapopata hizi tunawezesha watengenezaji wa mitambo kutoka duniani kutuletea mitambo ya uhakika wakijua kwamba tunazo pesa za kuwalipa, kwa hiyo hii ni mara ya kwanza tumezipata kwa mpigo, na tayari mitambo mbalimbali ya kutoa huduma bandarini iko njiani inakuja."

"Kwa hiyo tunatarajia baada ya kipindi kifupi kijacho, tutaona ufanisi wa bandari ukiongezeka mara dufu kwa sababu tutakuwa tuna teknolojia nyingi mpya na za kisasa, zenye uwezo wa kufanya kazi kwa ufanisi zaidi, kwa hiyo tutaokoa sana muda wa kuwahudumia wateja wetu," alisema.

Mushi alisema eneo jingine ambalo Bandari hiyo imepata mafanikio makubwa ni kwa serikali kutoa fedha za kuwalipa makandarasi.

# Chongolo: Dawa zisigeuzwe anasa

**Na Jacqueline Liana,**
SONGWE

KATIBU Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, ametahadharisha kuwa kama ukosefu wa dawa katika zahanati, vituo vya afya na hospitali, hautatafutiwa ufumbuzi, unaelekea kutengeneza mgogoro kati ya wananchi na chama hicho.

Akihitimisha ziara ya kikazi ya siku mbili mkoani Songwe, Chongolo amesema CCM haiwezi kuruhusu hali hiyo itokee kwa sababu kilitoa ahadi kupitia ilani ya uchaguzi ya 2020-2025, kwamba wananchi wakikichagua katika uchaguzi mkuu uliopita, kitahakikisha dawa zinapatikana katika taasisi hizo za kutoa tiba.

"Eneo la afya tuna changamoto, dawa zimekuwa kama anasa, hazifiki chini kwa wananchi, zinaelekea kutengeneza mgogoro kati ya chama chetu na wananchi, tutashughulikia," alisema Chongolo na kufafanua kwamba, licha ya mamilioni ya fedha kutolewa na serikali kwa ajili ya ununuzi wa dawa, malalamiko ya wananchi kuhusu ukosefu wa dawa ni mengi.

Kutokana na tatizo hilo, Chongolo aliahidi kukutana na taasisi za serikali zinazohusika na upatikanaji wa dawa katika zahanati, vituo vya afya na hospitali, ikiwa ni pamoja na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, pamoja na MSD, kufahamu ni kwanini mamilioni ya fedha zinazotolewa na serikali kwa ajili ya huduma hiyo, hazileti matokeo chanya, pia kupata suluhisho la kudumu la tatizo hilo haraka iwezekanavyo.

"Hili (la ukosefu wa dawa) tunalibeba tuweze kulishughulikia, na tutahitaji taarifa yenye kina itakayotoa suluhisho la tatizo hili," aliahidi Chongolo.

Katibu Mkuu Chongolo, alikuwa mkoani Songwe kwa ziara ya kikazi ya siku mbili iliyoanza Julai 9 hadi 10, kukagua uhai wa chama katika ngazi ya shina na utekelezaji wa ilani ya CCM.

Katika ziara hiyo, Chongolo amefuatana na Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa ya CCM (NEC), Kanali mstaafu Ngemela Lubinga, Katibu wa Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka na Katibu wa Umoja wa Vijana (UVCCM), Kenani Kihongosi.

Viongozi hao waligawana wilaya za kutembelea mkoani humo, na kila mmoja alilalamikiwa na wananchi katika ngazi ya shina kwamba madaktari wanawaandikia dawa, lakini hawazipati, na huambiwa wakanunue katika maduka ya dawa. Mathalani katika kijiji cha Chembe, kata ya Malangalali, wilayani Ileje, Kanali mstaafu Lubinga, alilalamikiwa na wananchi, licha ya kuwa na bima ya afya, wakiugua na kwenda kupata matibabu katika zahanati ya kijiji chao, dawa pekee wanayoambulia ni 'panadol'. Kuanzia leo Julai 11 hadi 13, 2021, viongozi hao waandamizi wa CCM, watakuwa na ziara ya kuhamasisha uhai wa Chama Cha Mapinduzi ngazi ya shina, pamoja na kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya CCM ya 2020-2025.




Wanafunzi wa Shule ya Feza Boys wakishangilia kwa kuwabeba wanafunzi wenzao waliofanya vizuri katika matokeo ya kidato cha sita na kuingia kumi bora, Harry Mshana na John Bugeraha. Shule hiyo ilishika nafasi ya sita (6) kitaifa baada ya kutangazwa kwa matokeo hayo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Operesheni punguza mahabusu' kuondoa msongamano

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeanzisha 'Operesheni Punguza Mahabusu' yenye lengo la kukabiliana na wimbi hilo itakayofanyika nchi nzima.

Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, Khamis Hamza Chilo, aliyasema hayo jana wakati akizungumza katika kikao kilichohusisha wafungwa na mahabusu wanawake waliopo katika Gereza la Ruanda, jijini Mbeya.

Katika kikao hicho kiongozi huyo alitoa msaada wa magodoro, taulo za kike, miswaki na sabuni kwa wafungwa.

"Miongoni mwa mambo ambayo Rais Samia Suluhu Hassan hapendi kuyaona ni mrundikano na ongezeko la watu katika jela hasa wanawake kwa kuwa anaamini ndiyo wanaojenga nchi na jamii wakishirikiana na wanaume, kikubwa tumeyachukua matatizo haya na tayari tunaanzisha operesheni maalumu itakayoitwa Operesheni Punguza Mahabusu," alisema.

Chilo alisema tayari serikali imeanza kuyaendea mbio baadhi ya mambo ikiwamo matatizo ya kuchelewa kwa upelelezi, utolewaji dhamana kwa kesi ndogo ndogo ambazo zinaongoza kwa kujaza mahabusu wengi katika magereza hali inayosababisha kuelemewa na mzigo mkubwa wa kuwalisha.

Mkuu wa Gereza la Wanawake, Mrakibu Mwandamizi wa Magereza, Rehema Mwailunga, alikiri kuwapo kwa msongamano unaosababishwa na Mkoa wa Mbeya kuwa na Mahakama ya Kanda.

"Mheshimiwa Naibu Waziri, ninashauri ili kupunguza msongamano tuone umuhimu wa kujenga bweni la wafungwa na mahabusu wa kike sambamba na hili lililopo hapa. Ninakiri msongamano huu unasababishwa na kuwapo kwa Mahakama ya Kanda hapa Mbeya hivyo mahabusu na wafungwa wengi kutoka magereza ya wilaya wanakuja kusikiliza kesi na rufaa zao hapa," alisema SSP Rehema.

# TARI kuzalisha miche mipya ya zabibu mil. 2

**Na Ashton Balaigwa**

TAASISI ya Kilimo Tanzania (TARI), Makutupora mkoani Dodoma, imejipanga kutekeleza agizo la Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, kwa kuzalisha miche milioni mbili kila mwaka ili kuwapatia wakulima wa mikoa inayolima zabibu kutokana na kuwapo soko la uhakika nchini.

Hayo yalisemwa na mtafiti wa mazao kutoka TARI Makutupora, Felista Mpole, wakati akitoa maelezo kwa wananchi waliotembelea maonyesho ya Sabasaba, Dar es Salaam, kuwa tayari wameanza uzalishaji wa zaidi ya aina 25 za miche vinasaba kwenye shamba mama lililopo mkoani Dodoma.

Alisema uamuzi ya serikali wa kukipa nguvu kilimo cha zabibu utasaidia kuongeza uzalishaji wa zao hilo nchini na kuwataka Watanzania kuchangamkia fursa ya kilimo cha zao hilo kutokana na kuwapo kwa soko la uhakika.

"Tumejipanga vizuri kuitikia agizo la serikali (Waziri Mkuu) la kuongeza tija katika kilimo cha zao zabibu, tunataka wakulima na wafanyabiashara wanaotaka kuwekeza kwenye kilimo hicho waje TARI Makutupora watapata miche ya kutosha ya zao hilo," alisema Mtafiti Felista.

Kwa mujibu wa mtafiti huyo, kati ya aina hizo uzalishaji wa zabibu hutumika kutengenezea mvinyo, kukausha kwa ajili ya matumizi mbalimbali kwenye vyakula pamoja na kula kama matunda ya kawaida ambayo soko kubwa bado lipo hapa.

Kwa upande wake mtafiti Armachius James, aliwakikishia wakulima na wafanyabiashara kuwa soko la zabibu nchini lipo la kutosha hasa kwenye maduka makubwa (Super Market) na zabibu za kitanzania kunawa na chupa mbili wakati zinazotoka nje zaidi ya aina 20.

Aliwataka wafanyabiashara kuwekeza kwenye kilimo cha zao hilo ili kusaidia kukuza uchumi wa nchi.

Naye, Mtafiti wa Uhaulishaji wa teknolojia kutoka kituo cha TARI Kihinga, kilichopewa jukumu la kuzalisha mbegu bora za michikichi, Kuzenza Madili, alisema hadi sasa wameshazalisha zaidi ya miche bora ya michikichi milioni tano na kuwapatia bure wakulima wa zao hilo mkoani Kigoma, ili kuongeza uzalishaji wake hatua ambayo itasaidia kupunguza kasi ya uagizaji wa mafuta kutoka nje ya nchi.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema timu ya watafiti kutoka taasisi hiyo kupitia vituo 17 wameweka kambi kwenye viwanja hivyo ili kuhakikisha inatoa elimu ya kilimo bora cha mazao ya mikakati kwa wakulima na wafanyabiashara wanaotaka kuwekeza katika kilimo hapa nchini ili kuzalisha kwa tija.

Alisema wakulima na wafanyabiashara ambao watanufaika na teknolojia hizo ni kutoka mikoa ya Morogoro, Pwani, Tanga, Iringa na Dar es Salaam na kituo hicho kitatoa huduma hizo kwa siku zote.

# Doto James aagiza mafunzo wafanyakazi TBS

**Na Beatrice Moses**

KATIBU Mkuu wa Wizara ya Viwanda na Biashara, Dotto James, ameiagiza Bodi ya Shirika la Viwango Tanzania (TBS) kuhakikisha inaanda mpango wa mafunzo kazini ndani na nje ya nchi kwa wafanyakazi wa shirika hilo yatakayowawezesha kwenda sambamba na teknolojia ya vifaa vya kisasa wanavyovitumia.

Katibu Mkuu huyo alitoa agizo hilo mwishoni mwa wiki wakati wa hafla ya Waziri wa Viwanda na Biashara, Prof. Kitila Mkumbo, akizindua bodi mpya ya TBS ambayo mwenyekiti wake ni Dk. Fenela Mkangara.

James alisema kati ya taasisi 10 nyeti za serikali zinazofanyakazi kwa kutumia vifaa vya teknolojia ya kisasa, TBS haiwezi kukosekana na imekuwa na wafanyakazi waliobobea. "TBS ina wataalamu waliobobea na vifaa vya kisasa na toshelevu, hivyo ni muhimu vitengo vyote viwe na wataalamu angalau watano kila kimoja ili hata vifaa vya teknolojia ya kisasa vinavyotumiwa na shirika hilo vikiharibika, wawepo watu wa kuvitengeneza," alisema James.

Alisema kuwa na mtaalamu mmoja ambaye akienda likizo au kustaafu na kuamua kumwongezea mkataba kwa ajili ya kufanya matengenezo ya vifaa vinapoharibika kumepitwa na wakati, na kwamba hakuna sababu ya shirika kutumia gharama kubwa kulipa wataalamu kutoka nje.

"Kwa hiyo mtenge bajeti kwa ajili ya mafunzo kazini ili pale vifaa vinapoharibika tuwe na wataalamu wa kutosha, wastani wa wataalamu watano kila kitengo, sio mtu anaenda likizo au anastaafu mnamwongezea mkataba," alisema James.

Kwa upande wake, Prof. Mkumbo, aliwataka wajumbe wa bodi hiyo kuhakikisha wanakuwa na uelewa mpana na uwezo wa kufanyakazi kwa mujibu wa sheria iliyoanzisha bodi hiyo.

Alisema wakati wa uteuzi wa bodi hiyo sifa za kutosha zilihitajika, hivyo serikali inatarajia mijadala yenye afya na hata wakitofautiana, watofautiane bila kugombana ili maamuzi yawe yenye maslahi.

Kwa mujibu wa Waziri Mkumbo, suala la viwango ni jambo kubwa, hivyo wanahitaji kuona kila jambo linalofanyika linazingatia sheria.

Alisema jukumu kubwa la serikali ni kuandaa sera, kanuni, miongozo na usimamizi wa jumla wa shirika.

"Kwa hiyo kazi ya bodi ni kuhakikisha malengo yanayotolewa na serikali yanafikiwa, hivyo ni muhimu bodi kuwa mtekelezaji wa maelekezo ya serikali," alisisitiza.

Prof. Mkumbo alisisitiza kwamba kazi ya bodi hiyo ni kulinda maslahi ya mwenye shirika, ikiwa ni pamoja na kutetea maslahi ya wadau.



Mkurugenzi Mtendaji wa TBL Plc, Jose D Maron, akiwaeleza wajumbe wa Kamati ya Bunge ya Viwanda na Biashara juu ya shughuli za kampuni wakati walipotembelea kiwanda cha bia cha Ilala mkoani Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Benki itakavyowanufaisha vijana kwenye ujasiriamali

**Na Enock Charles**

BENKI ya KCB Tanzania imeazimia kutoa mikopo yenye riba nafuu ya kuanzia shilingi milioni 5 na kuendelea kwa wajasiriamali ambao wamehitimu Programu ya Mafunzo ya ujasiriamali kwa vijana awamu ya pili ya benki hiyo.

Watapatiwa mikopo hiyo ikiwa watawasilisha mipango ya biashara iliyoandikwa vizuri. Akizungumza wakati wa kufunga semina elekezi kwa vijana wajasiriamali 118 ambao ni sehemu ya vijana 300 kutoka mikoa sita iliyofanyika Dar es Salaam mwishoni mwa wiki, Mkuu wa Masoko na Biashara wa KCB, Christina Manyenye, alisema ni wajasiriamali tu ambao wataandika mipango ya biashara makini pekee ndiyo watanufaika na mikopo hiyo.

"Tumewaalika kuwasilisha mipango yao ya biashara na wenye mipango mizuri watapata mkopo wa Sh. milioni 5- na zaidi kulingana na maandiko yao. Programu hii imewahusisha vijana 300 waliohitimu kutoka mikoa ya Dar es Salaam, Arusha, Kilimanjaro, Morogoro, Mwanza na Zanzibar. Hatua inayofuata ni kuwaunganisha na viwanda vya kusindika na kuchakata kwa kipindi cha miezi sita kupata ujuzi zaidi wa vitendo," alisema Manyenye.

Mbali na mikopo ya kukuza biashara zao ndogo, Manyenye alisema wafanyabiashara wachanga watapewa wataalamu watatu kwa kila mmoja katika maeneo ya masoko, sheria na wahasibu kutoka benki hiyo ambao watachukua jukumu la kuwashauri juu ya njia nzuri za kuendesha biashara zao, kuzihudumia, kutafuta masoko ya bidhaa zao na kuandaa taarifa za kifedha.

Peter Sona, mmoja wa wanufaika wa programu hiyo na mhitimu wa teknolojia ya habari na mawasiliano (ICT), alisema maarifa yanayopatikana katika vyuo vikuu na vyuo vya kati hayatoshi kuwafanya wahitimu kuwa na uwezo thabiti unaohitajika na soko la ajira.

Benki ya KCB imetumia shilingi milioni 100 kwa ufadhili wa kozi hiyo. Mpango huo unatekelezwa kwa kushirikiana na Baraza la Kitaifa la Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi (NEEC). Pia ina walimu na wakufunzi kutoka Shirika la Kuendeleza Viwanda Vidogo (SIDO).

# TRA yawahimiza w'biashara risiti

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

MAMLAKA ya Mapato (TRA), Mkoa wa Kagera imewataka wafanyabiashara kutoa risiti kwa wateja wanaofanya manunuzi ya bidhaa ili kusaidia kuongeza makusanyo na kufikia lengo lililopangwa na serikalini.

Meneja wa TRA mkoani humo, Adam Ntoga, alisema hayo wakati akitoa taarifa ya ukusanyaji wa mapato kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2020/2021 na jinsi walivyoweza kuvuka lengo na kukusanya Sh. bilioni 73.1 badala ya Sh. bilioni 71 walizokuwa wakikusanya.

Ntoga alisema wapo wafanyabiashara wasio waaminifu, ambao wanatoa risiti zisizokuwa halali kwa wateja wanaofanya manunuzi bila kutambua kuwa huo ni ukiukwaji wa taratibu za mamlaka.

"Kuna wengine wanachouza hakiendani na thamani kwenye utowaji wa risiti za manunuzi kwa wateja wao ambao wanufaika kwa kupata huduma unakuta manunuzi yamefanyika ya Sh. milioni 1, lakini kwenye risiti imeandikwa Sh. 100,000," alisema Ntoga.

# TADB yateua miradi wilaya Kanda ya Ziwa

**Na Mwandishi Wetu**

MIKOA ya Mwanza, Kagera na Mara imeteua miradi inayopata mikopo ya Benki ya Kilimo Tanzania (TADB) na kutekelezwa katika wilaya za Misungwi, Nyamagana, Ngara, Tarime na Roya ili izinduliwe na ujumbe wa Mwenge wa Uhuru.

Hiyo inatokana na umuhimu wa miradi hiyo katika kukuza uchumi wa wilaya husika na kubadili maisha ya wananchi. Miradi yote imeshapokea mikopo ya masharti nafuu kutoka TADB.

Katika taarifa yake kwa vyombo vya habari jana juu ya uteuzi wa miradi hiyo, kila mradi umepokea fedha kulingana mahitaji yaliyoainishwa ili uimarike na uwezo wake wa kukuza kipato cha wakulima na kuleta mapinduzi katika wilaya husika. Imeitaja miradi hiyo ni

Authur Mgongo Poultry Farm, ambao unatekelezwa katika wilaya za Misungwi na Nyamagana na kueleza kwamba umeteuliwa kwa sababu ni wa kisasa na uongozi wa Mkao wa Mwanza umeuteua kuwa shamba darasa kwa wafugaji wadogo wa kuku ili wapate mbinu za kisasa za ufugaji wa kuku.

"TADB imetoa shilingi milioni 300 kwa ujenzi wa nyumba na vizimba ili ufugaji uwe wa kileo. Halmashauri ya Wilaya ya Nyamagana inatumia mradi huu kuwa ni taasisi mahususi ya wanafunzi kujifunza ufugaji wa kisasa wa kuku," imeeleza.

Mradi wa kuzalisha miche bora ya mibuni ndiyo wa kwanza katika Wilaya ya Ngara, Mkoa wa Kagera, na unatarajiwa kuzalisha miche milioni moja ili isambazwe kwa wakulima kwa lengo la kuongeza wingi na ubora wa buni zivunwazo na kahawa inayonywewa. Mradi huo unatarajiwa kuongeza wingi na ubora wa kahawa ya robusita na arabica.

## Kanzidata ya wataalamu wa mafuta kuzinduliwa

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mkondo wa Juu wa Petroli (PURA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) inatarajia kuzindua kanzidata ya wataalamu wa sekta hiyo Julai 15, mwaka huu.

Kanzidata hiyo inatarajiwa kujumuisha wataalamu, wauzaji na watoa huduma katika sekta ya petroli na gesi ili kuwezesha wawekezaji wa ndani na nje kupata wataalamu sahihi na washirika watakaofanya sekta hiyo kukua zaidi.

Akizungumza katika Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF) Mkuu wa Kitengo cha Ushirikishaji wa Wazawa na Ujumuishaji wa Wadau kutoka PURA, Charles Nyangi, alisema tayari mamlaka hiyo imepewa kibali cha kuanzisha kanzidata hiyo kwa wauzaji na watoa huduma kwa ajili ya wawekezaji kupata wataalamu sahihi ikiwa ni pamoja na wahandisi wa mafuta ya petroli, wasambazaji, watoa huduma pamoja na washirika wa biashara za mafuta na gesi.

"Kanzidata hiyo itakuwa na taarifa zote zinazohitajika ambazo ni pamoja na wataalamu katika sekta hiyo, na tumeweka sifa zao za awali na kwa usahihi ili kurahisisha hata kwa wawekezaji kupata wataalamu kwa urahisi wanapokuja nchini kuwekeza," alisema Nyangi.

## Washauriwa kuhusu matumizi ya mbolea

**Na Elizabeth Zaya**

MAMLAKA ya Udhibiti wa Mbolea Tanzania (NFRA), imewataka wakulima nchini kuzingatia matumizi sahihi ya mbolea ili iwasaidie kulima na kuzalisha kwa tija.

Ushauri huo ulitolewa jana na Ofisa Udhibiti Ubora wa Mbolea kutoka mamlaka hiyo, Michael Sanga, wakati akizungumza katika banda lao kwenye Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF).

Sanga alisema upo umuhimu wa kuzingatia namna ya kutumia mbolea kwa ubora kwenye kilimo na kwamba pasipo kufanya hivyo, mkulima huenda asione manufaa kupitia shughuli zake za kilimo hicho.

Alisema kabla ya mkulima kutumia mbolea anapaswa kwanza kupima afya ya udongo katika eneo analolima ili kufahamu aina na kiasi cha virutubisho vilivyomo katika udongo husika na hivyo kutumia inayoendana nao.

"Na huduma hizi zote ikiwamo za ushauri wa namna ya kutumia mbolea kwa usahihi zinatolewa na NFRA katika kanda zote nchini, kwa hiyo tumekuwa tukiwashauri wakulima kwamba ni vema wasipende kutumia ovyo mbolea hizi, wapende kwanza kupata ushauri na ndipo watafaidika zaidi na shughuli za kilimo," alisema Sanga.

Jambo jingine ambalo alisema wanapaswa kuzingatia ni aina ya mazao wanayopaswa kulima kulingana na aina ya udongo na kwamba kila zao huwa lina asili ya kuhitaji virutubisho vya aina yake.

# PPRA yataka 30% bajeti ya ununuzi kwa makundi maalum

**Na Mwandishi Wetu**

MAMLAKA ya Kudhibiti Ununuzi wa Umma (PPRA), imezitaka taasisi za ununuzi kuhakikisha zinazingatia matakwa ya Sheria ya Ununuzi wa Umma kwa kutenga asilimia 30 ya bajeti ya ununuzi ya mwaka, kwa ajili ya makundi maalum.

Akizungumza na waandishi wa habari katika banda la Mamlaka kwenye Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa maarufu kama 'Sabasaba', Kaimu Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Mhandisi Mary Swai, amesema ni muhimu kuwahimiza wananchi wenye sifa kujiunga kwenye makundi na kusajiliwa kama wanufaika wa upendeleo wa makundi maalum.

Aidha, alisema mwaka huu wa fedha, PPRA imetenga bajeti ya kuendesha mafunzo kwa ajili ya makundi maalum yanayotajwa kwenye sheria, ambayo ni wanawake, vijana, wazee na watu wenye ulemavu.

Akizungumzia vigezo vya kikundi cha walengwa kusajiliwa na kutambuliwa kama kundi maalum linalopaswa kufaidika na asilimia 30 ya bajeti ya taasisi nunuzi, alisema sheria inataka asilimia 70 ya wajumbe wa kundi hilo kuwa na sifa za kundi husika.

"Mtu akisajili kikundi ni lazima asilimia 70 ya wanachama wawe ni wa kundi husika. Sio tunasema ni kundi la wanawake halafu ukute wanaume wenzao ndio wanaoliongoza. Ili kuwa na mchanganyiko na kundi liwe na sifa, labda wanaume wawe ni asilimia 30 na wanawake asilimia 70," alisema Mhandisi Swai.

"Pia, kwenye upande wa uongozi wa kundi, ni lazima asilimia 100 ya uongozi iwe na wajumbe wa kundi husika. Kwa hiyo kama ni kundi la wanawake, viongozi wote wanapaswa kuwa wanawake. Kama ni kundi la wenye ulemavu, viongozi wote wanatakiwa kuwa ni wa kundi la walemavu," aliongeza.

Aliwahimiza wananchi kutembelea banda la PPRA kwenye maonesho hayo, kutembelea ofisi za PPRA na kufuatilia kwa karibu taarifa zinazotolewa, ili waweze kuwa sehemu ya watakaofaidika na mafunzo yatakayoanza kutolewa hivi karibuni.

Kwa mujibu wa mwongozo uliotolewa na PPRA, asilimia 30 ya bajeti ya mwaka ya ununuzi ya taasisi husika inayotengwa kwa ajili ya makudi maalum, hugawanywa kwa asilimia 10 kwa ajili ya kundi la wanawake, asilimia 10 kwa ajili ya vijana, na makundi mengine ya wazee na watu wenye ulemavu hupata asilimia 5 kila moja.




Ofisa Mtendaji Mkuu wa PPRA, Mhandisi Mary Swai, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) katika Banda la PPRA kwenye Maonyesho ya Sabasaba jijini Dar es Salaam juzi. **MPIGAPICHA WETU**

# Biashara, kampuni 200 zasajiliwa Sabasaba

**Na Elizabeth Zaya**

WAKALA wa Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) imesema tangu kuanza kwa Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara Dar es Salaam (DITF), imesajili majina ya biashara na kampuni zaidi ya 200.

Mkuu wa Kitengo cha Habari na Mawasiliano wa BRELA, Roida Andusamile, alisema usajili huo umekuwa ukifanyika kwa njia ya mtandao, lakini wametoa ofa katika kipindi hiki cha maonyesho kwa watu kufika katika banda lao na kusajiliwa moja kwa moja.

"Usajili wa kampuni na majina ya biashara BRELA hufanyika kwa njia ya mtandao, lakini tumeona tutoe ofa maalum katika kipindi hiki cha maonyesho kuwasajili wale wote wanaokuja kututembelea," alisema Roida.

"Na wapo baadhi ambao wamekuwa wakipata changamoto ya namna ya kujisajili kwa njia ya mtandao hususani wale wanaokuwa hawana barua pepe, kwa hiyo wakija hapa tunawaelekeza namna ya kufungua barua pepe zao na tunawapa akaunti namba zetu maana unapojisajili lazima upate na akaunti namba," alisema Roida.

Mbali na usajili, alisema wametumia kipindi hiki cha maonyesho, kutoa ushauri na elimu kwa wale ambao walikuwa hawafahamu namna wanavyofanya kazi zao.

"Na tumepata idadi kubwa sana ya wanaliokuja kujisajili na kutafuta kuelimishwa kuhusu namna ya kujisajili, lakini kufahamu namna BRELA inavyofanya kazi. Karibu kila siku tangu kuanza kwa maonyesho haya tunaondoka saa mbili usiku kutokana na wingi wa watu, wakati katika mabanda mengine saa 12 jioni tu wanakuwa wameshafunga," alisema.

"Hii inatia moyo sana na inaonyesha ni kwa namna gani Watanzania wamehamasika katika kuingia kwenye biashara na ni jambo la kujivunia kiukweli na tunaami mpaka mwisho wa maonyesho tutakuwa tumesajili majina ya biashara na kampuni zaidi ya 500."

Alisema katika idadi hiyo ya watu wanaojitokeza kusajili kampuni na majina ya biashara, wanawake nao wameonyesha mwitikio mkubwa sana.

"Na kitu kingine ambacho tumejivunia kwa awamu hii ya maonyesho ya 45, tumeona idadi kubwa sana ya wanawake wamekuja kusajili kampuni zao na majina ya biashara zao, tunalipongeza kundi hili kwa hamasa waliyonayo kwenye masuala ya biashara," alisema Roida.

Nipashe
Spotika



WALINZI 10 BORA LALIGA MSIMU WA 2020-21 UK. 12-13



# KANE, POGBA KUVUNJA REKODI YA USAJILI?

**LONDON, England**

MACHO yote huenda yameelekezwa katika kilele cha Euro 2020, lakini huku msimu mpya ukiwa umbali wa mwezi mmoja pekee, klabu zipo katika harakati za kuwasajili wachezaji wapya.

Manchester United ilianza kwa kumsajili Jadon Sancho kwa uhamisho wa dau la pauni milioni 73, lakini je, ni mchezaji gani mwengine ambaye anahamia klabu nyengine? Je, nyota wa Euro atahamia katika Ligi Kuu ya England?

Wachezaji wawili ambao huenda wakavutia kiasi kikubwa cha fedha katika uhamisho wao ni mshambuliaji wa England, Harry Kane na Jack Grealish wote wakinyatiwa na Manchester City.

Kane mwenye umri wa miaka 27, ameweka wazi kwamba anataka kuondoka katika klabu ya Tottenham ambayo haijakubali kumwachilia mchezaji ambaye ana kandarasi ya miaka mitatu iliyosalia.

Ukweli ni kwamba klabu hiyo ilimwambia kocha wake mpya, Nuno Esporito Santos kwamba inataraji kwamba nahodha huyo wa klabu ya England atasalia.

Aston Villa nayo inatumia fursa yake ya kumzuia kiungo wake wa kati Grealish mwenye umri wa miaka 25, lakini ni watu wachache wanaotarajia kwamba watafaulu.

Imekataliwa na washikadau wote lakini kuna uvumi kwamba makubaliano ya Grealish kuichezea Man City msimu ujao yameafikiwa.

Beki wa kati wa England, Ben White mwenye umri wa miaka 23, huenda akajiunga na Arsenal huku Brighton ikitarajiwa kupata malipo mazuri hususan baada ya kumwongezea mkataba msimu uliokwisha.

West Ham imeweka wazi kwamba haipo tayari kumuuza kiungo wa kati wa England, Declan Rice lakini hiyo haimaanishi kwamba haitamuuza.

Na iwapo West Ham huenda wakamkosa Rice, je, Leeds haipo katika hali kama hiyo inapokaribia kumpoteza kiungo wao wa kati wa England, Kalvin Phillips mwenye umri wa miaka 25?

Baada ya kukosa michuano ya Euro kutokana na ukosefu wa kushiriki katika mechi, kiungo wa kati, Harry Winks mwenye umri wa miaka 25, huenda akaondoka klabu ya Tottenham.

Na iwapo Kane na Grealish watawasili katika klabu ya Man City, kutakuwa na wachezaji ambao wataondoka katika klabu hiyo huku hatma ya mshambuliaji wa Brazil, Gabriel Jesus mwenye umri wa miaka 24, kiungo wa kati wa Ureno, Bernardo Silva mwenye umri wa miaka 26, zikiwa hazijulikani.

Vilevile kumekuwa na uvumi kuhusu kiungo wa kati wa Man United na Ufaransa, Paul Pogba tangu alipojiunga na klabu hiyo ya Old Trafford 2016.

Kiungo huyo wa Ufaransa mwenye umri wa miaka 28 amefanya mazungumzo na United kuhusu kuongeza kandarasi yake inayokamilika 2022.

Iwapo hatatia saini kandarasi mpya, United huenda ikampoteza kama mchezaji huru chini ya kipindi cha miezi kumi na mbili au kujaribu kumuuza katika soko lilolo na shinikizo kuu kwa chini ya pauni milioni 89 walizolipa ili kumsajili.

Lakini iwapo atatia saini kandarasi mpya, huenda akaongezewa mshahara wakati ambapo wengi wanahoji iwapo anahitaji kuongezwa mshahara huo.

Wakati huohuo, United imewasiliana na Real Madrid kuhusu beki na mshindi wa kombe la dunia na Ufaransa, Raphael Varane.

Kandarasi ya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 inakamilika mwisho wa msimu ujao na kuna wasiwasi wa iwapo ataongezewa kandarasi ambayo itafikia mahitaji yake, huku Real ikiaminika kutaka kumuuza kwa pauni milioni 50.

Mbali na Ligi ya England, Lionel Messi, 34, anatarajiwa kusalia katika klabu yake Barcelona, licha ya kuwa mchezaji huru baada ya kandarasi yake kukamilika.

Mazungumzo kuhusu Christiano Ronaldo kutaka kurudi katika klabu ya Man United yanaendelea, lakini itagharimu kitita kikubwa cha fedha.

Manchester City na Paris St-Germain zina uwezo wa kufanya usajili mkubwa kutokana na hali yao ya kifedha ambayo imewalinda dhidi ya janga la corona.

Kwa wengine, ni swali la kutumia fedha vilivyo.

Hatua hiyo inaweza kufanyika kupitia ufadhili, kama Man United ilivyofanya, kuuza hisa, kama walivyofanya Juventus Jumatano iliopita, kuomba mkopo ama kuuza mali yake, hatua inayomaanisha kuuza wachezaji, ardhi ama nyumba.

Ni msemo maarufu kwamba klabu kutokana na mchezo wao mzuri pekee katika michuano mikubwa.

## ISIKUPITE

GOLIKIPA Namba 1 wa Simba na Timu ya Taifa, Taifa Stars, Aishi Manula, anaongoza kwa kucheza mechi 17 kwenye Ligi Kuu bila kuruhusu wavu wake kuguswa maarufu kama 'clean sheets'.



## Extra Time

# WALINZI 10 BORA LALIGA MSIMU WA 2020-21



GERARD PIQUE



RAMOS

**MADRID, Hispania**

MSIMU wa 2020-21 kwenye Ligi Kuu ya Hispania, LaLiga, ulimalizika kwa aina yake, huku Atletico Madrid wakitwaa taji hilo kwa mara ya 11 katika historia yao.

Kikosi hicho cha kocha, Diego Simeone, kilipambana kutoka nyuma na kulitwaa taji hilo kwa kuifunga Real Valladolid 2-1, huku Luis Suarez aliyetupia virago kule Barcelona akifunga la ushindi.

Klabu yake ya zamani ilimaliza nje ya mbili bora kwa mara ya kwanza kwa kipindi cha miaka 13, huku Real Madrid wakishika nafasi ya pili.

Lionel Messi alimaliza kama mfungaji bora wa ligi hiyo ikiwa ni mara ya nane, akifikisha mabao 30.

**Makala haya inawaangalia walinzi bora 10 wa LaLiga kwa msimu wa 2020-21:**

**#10 Emerson Royal (Real Betis)**

Real Betis ilifuzu kucheza Ligi ya Europa, lakini wanaweza wakashiriki katika mashindano hayo msimu unaokuja bila ya mmoja wa wachezaji wake muhimu. Emerson Royal, ambaye alikuwa akicheza kwa mkopo kule Barcelona na inaonesha hakuna uwezekano wa kurudi katika klabu yake mama.

Kwa sababu mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil alikuwa na msimu mzuri na kiwango cha kuvutia. Alichangia bao moja na kutoa pasi za mwisho nne kwa Los Verdiblancos hao, lakini akifanya kazi kubwa zaidi kwenye safu ya ulinzi.

#9 Sergio Ramos (Real Madrid)

Sergio Ramos anaweza akawa hajashinda tuzo nyingine nje ya Santiago Bernabeu, lakini umuhimu wake kwa Real Madrid ni mkubwa mno. Mkongwe huyo ameshaondoka hapo Madrid na ametua kule PSG ambako anaweza kumalizia soka lake.

Kwa kipindi cha miaka 16 alichocheza Real Madrid mchango wake umekuwa ni mkubwa zaidi na sasa atakuwa akiendelea kuonesha umwamba wake kule kwenye viunga vya jiji la Paris.

**#8 Gerard Pique (Barcelona)**

Msimu wake huo ulikuwa umemzonga kwa majeruhi na kiwango chake kimeonekana kuporomoka tangu mwaka jana. Lakini Gerard Pique anabakiwa kuwa mchezaji muhimu zaidi kwa Barcelona timu ambayo amekuwa nayo kwa karibia muongo mmoja uliopita.

Katika mechi 18 LaLiga alizoanza msimu uliopita, raia huyo wa Hispania alionekana kuwa kwenye kiwango cha kuvutia. Pasi zake zilikuwa za uhakika kwa asilimia 94. Na sasa Pique anaonekana anaweza kucheza kwa miaka michache tu hapo Barcelona, kwani sasa umri unamtupa mkono.

**#7 Jose Gaya (Valencia)**

Ni rahisi kusahau kwamba, Jose Gaya ndio kwanza ana umri wa miaka 25 wakati alipokuwa akicheza msimu wake wa tisa kwa Valencia. Lakini ulikuwa msimu wake mwingine bora zaidi kwenye LaLiga, huku mlinzi huyo wa pembeni alitoa pasi za mwisho saba, zikiwa nyingi zaidi kwa mlinzi.

Gaya kwa sasa anakodolewa macho na Barcelona ambao wanamuona anaweza kuwa msaada kwao kwenye nafasi ya ulinzi.

**#6 Ferland Mendy (Real Madrid)**

Ferland Mendy alikosa mechi nane za mwisho za LaLiga, lakini ubora wake unazungumza vizuri tu, kwani alimuweka benchi Marcelo na yeye kuwa chaguo la kwanza kwenye timu. Kwa uhakika Mendy amekuwa kwenye kiwango cha kuvutia zaidi tangu alipojiunga na Real Madrid mwaka 2019 na aliendelea kuwa bora kwa msimu wa 2020-21.

Usaidizi wake kwenye mashambulizi pia ulikuwapo, akifunga bao moja kwenye LaLiga huku akiwa hajatoa pasi yoyote ya mwisho. Lakini Mendy alikuwa mchezaji muhimu kwa kuzuia mashambuliji katika safu ya ulinzi ya Real Madrid. Lakini bahati mbaya alikumbwa na majeruhi, ambapo raia huyo wa Ufaransa alikosa mechi chache za Ligi msimu huu.

**#5 Jordi Alba (Barcelona)**

Jordi Alba alionesha ubora wake wa kuvutia sana, huku akifunga mabao matatu na kutoa pasi za mwisho saba kwenye LaLiga, na hakika alithibitisha ubora wake kwa Barcelona.

Katika mechi za mwisho za LaLiga, Alba alikuwa akicheza zaidi katika nafasi ya kiungo wa kushoto na alionesha umuhimu wake mkubwa.

**#4 Keiran Trippier (Atletico Madrid)**

Kieran Trippier alikuwa mmoja ya nguzo imara kwa Atletico Madrid wakati wakishinda taji la Ligi licha ya kukosa mechi 10.

Baada ya kuiwakilisha England kwenye kombe la Dunia mwaka 2018, ambapo England ilifika nusu fainali, Keiran Trippier akajiunga na Atletico Madrid mwaka 2019. Na sasa ametwaa taji lake la kwanza kubwa katika maisha ya soka.

Mchezaji huyo wa zamani wa Tottenham Hotspur, alikuwa na kiwango cha kuvutia kwenye safu ya ulinzi. Kwa maneno mengine, Trippier alikuwa nguzo kwa kikosi cha Simeone kilichoshinda taji lake la kwanza la LaLiga kwa kipindi cha miaka saba licha ya kukosa mechi kadhaa.

**#3 Jules Kounde (Sevilla)**

Jules Kounde alikuwa na msimu mzuri sana wa 2020-21. Yeye ni mmoja wa walinzi bora kabisa wa Ufaransa. Na Kounde alitengeneza ubora wake katika msimu wake wa kwanza kwenye LaLiga kwa kujiimarisha yeye menyewe kwa kiwango cha kuvutia kabisa.

Kounde pia alikuwa msaada wa kutengeneza mashambulizi kwani alifunga mabao mawili na kutoa pasi za mwisho mbili. Katika umri wake wa miaka 22, ana nafasi ya kuendelea kuwa bora zaidi na zaidi.

**#2 Stefan Savic (Atletico Madrid)**

Kuondoka kwa Diego Godin mwaka 2019 kuliacha mlango wazi kwa Stefan Savic. Nyota huyo wa Montenegro amekuwa nguzo muhimu kwenye safu ya ulinzi tangu wakati huo.

Mafanikio ya Los Rojiblancos hao kwa mara nyingine pia yalijengwa na Savic, kwani alikuwa nguzo imara zaidi kwa kuzuia mashambulizi langoni mwake. Hata hivyo, nidhamu yake mbovu ilimfanya kutokuwa na maelewano mazuri na Diego Simeone.

**#1 Pau Torres (Villarreal)**

Villarreal walikuwa na bahati mbaya ya kukosa kufuzu michuano ya Ligi ya Europa baada ya kufungwa na Real Madrid kwenye mchezo wa mwisho wa Ligi msimu uliopita. Lakini wasingeweza kufika mbali bila kiwango bora cha Pau Torres na kuimarisha safu yao ya ulinzi.

Torres alijiimarisha yeye mwenyewe kama mmoja wa walinzi bora zaidi kwa kikosi hicho na kwa vyovyote ana nafasi nyingine ya kutamba msimu unaokuja.

Klabu za Arsenal na Manchester United ziliripotiwa kuwania saini yake, na wanaweza kuongeza juhudi zao kumwania kipindi hiki cha dirisha la kipindi cha majira ya joto.

## Nukuu

"Nilikutana na viongozi nimewaeleza kwamba nataka iundwe kamati ya usajili ambayo watashirikiana na maskauti ambao nimewaeleza ila kupata wachezaji ambao watasaidia kufikia malengo yetu kwa msimu ujao," **Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi akizungumzia usajili wa timu yake.**




"Hadi sasa tumekamilisha usajili wa nyota wawili; Charles Edward Manyama na Charles Zulu ambao wamesaini mkataba na msimu ujao kuonekana katika viunga vya Azam Complex, Chamazi, **" Mtendaji Mkuu wa Azam FC, Abdulkarim Amin 'Popat' akizungumzia usajili.**



"Diego Pablo Simeone amesaini mkataba mpya ambao utamweka hadi Juni 30, 2024. Tangu raia huyu wa Argentina alipojiunga na klabu mwaka 2011, tumefurahia kwa pamoja mafanikio makubwa kwa klabu na kushinda mataji,**" Taarifa ya Klabu ya Atletico Madrid baada ya kumpa mkataba mpya kocha wake, Diego Simeone.**





Aishi Manula-Simba

# MAKIPA WABONGO WAFUNIKA LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI Ligi Kuu Tanzania Bara ikielekea ukingoni, makipa wa Kitanzania wameonekana kufanya kazi kubwa sana, wakiwa bora zaidi, tofauti na miaka kadhaa iliyopita ambapo ligi ilikuwa inatawaliwa na wanaotoka nje ya nchi.

Kwa misimu kadhaa nyuma, Simba, Yanga na Azam zilikuwa zinapigana vikumbo kusaka makipa kutoka nje ya nchi, lakini jinsi ilivyo kwa sasa hali imeanza kubadilika.

Hata timu nyingine za Ligi Kuu, zilikuwa zinasajili makipa kutoka nje ya nchi, huku wa Kitanzania wakiwa hawaaminiki sana.

Kwa sasa Wabongo wengi nao wameonekana kuwa na viwango vya hali ya juu kuwazidi hata wa nje.

Angalau makipa wa nje wachache waliobaki wanatamba ni Mathias Kigonya wa Azam ambaye ni raia wa Uganda, Jonathan Nahimana, Mrundi anayeichezea Namungo na Nurdin Balora raia wa Ghana.

Kama makipa wa Kibongo wakiendelea hivi, misimu michache nyuma, inaweza kushuhudia kusiwe na kipa kutoka nje ya nchi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Hakuna timu inayotaka kipa nje ya nchi wakati wapo makipa bora nchini.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu ni kwamba makipa wengi wa Kitanzania ndiyo wanaongoza kwa kucheza mechi nyingi bila kuruhusu bao, maarufu kwa wanamichezo kama 'clean sheets.'

Kwenye makala haya, tutawaangalia makipa wenye 'clean sheets' nyingi kwenye Ligi Kuu mpaka sasa.

**1. Aishi Manula-Simba**

Ndiye kipa namba moja wa timu ya Simba na Timu ya Taifa ya Tanzania, Taifa Stars. Alijiunga na timu hiyo msimu wa 2017/18 na tangu atue amekuwa akiipa ubingwa.

Amekuwa akikaa langoni kwenye mechi nyingi katika timu yake ya Simba kwenye Ligi Kuu, Ligi ya Mabingwa Afrika, Kombe la FA, wakati mwingine hata kwenye mechi za kirafiki.

Manula kipa Mtanzania ndiye anayeongoza kwa kuwa na 'clean sheets' nyingi kuliko makipa wote mpaka sasa.

Amesimama mechi 17 bila kuruhusu bao.

Atakayemaliza Ligi Kuu msimu wa 2020/21 akiwa na 'clean sheets' nyingi kutokana na makipa wote waliobaki timu zao kubakisha mechi mbili tu.

**2. Metacha Mnata-Yanga**

Kipa mwingine Mtanzania ambaye anashika nafasi ya pili kwa kuwa na 'clean sheets' nyingi kwenye Ligi Kuu.

Ana 'clean sheets' 13 mpaka sasa ingawa hakuna uhakika tena wa kuongeza kwani amesimamishwa na klabu yake ya Yanga kwa sasa kutokana na madai ya utovu wa nidhamu.

**3. Aboutwalib Mshery-Mtibwa Sugar**

Pamoja na Mtibwa Sugar kusuasua kwenye Ligi Kuu, lakini kipa wake Aboutwalib Mshery ameingia kwenye orodha ya makipa kwenye 'clean sheet' nyingi kwenye ligi, naye akiwa na 13 kama ilivyo kwa Metacha.

Huyu ni kipa kinda kabisa na ni hazina kuwa kwa taifa la Tanzania baadaye.

**4. Haroun Mandanda-Mbeya City**

Timu yake ya Mbeya City haiko sehemu salama, lakini takwimu zinambeba kipa huyo Mtanzania akiwa na 'clean sheets' 13 mpaka sasa, kama Metacha na Mshery.

Mandanda amekuwa mmoja wa makipa bora kabisa kwenye Ligi Kuu msimu huu.

**5. Jeremiah Kisubi-Prisons**

Kisubi ni mmoja wa makipa bora ambaye Tanzania imejaliwa kuwa nao. Huu ni msimu wake bora kabisa, licha ya kuwahi kuzidakia klabu za Ndanda na Kagera Sugar.

Ni mmoja wa makipa wachache ambao wana mbwembwe sana wakaapo golini. Zamani aina hii na makipa nchini walikuwa wengi, lakini kwa sasa wamepotea.

Ameidakia Prisons msimu huu kwa mafanikio makubwa, kiasi kwamba klabu mbalimbali kubwa zimekuwa zikimnyemelea. Kuna tetesi kuwa huenda akatua kwenye klabu ya Simba Ligi Kuu Tanzania Bara ikatapomalizika.

**6. Juma Kaseja-KMC**

Huyu ni kipa mkongwe nchini kuliko wote wanaocheza Ligi Kuu kwa sasa. Alianza kucheza Ligi Kuu mwaka 2001 akiwa na klabu ya Moro United, kabla ya kujiunga na Simba mwaka 2002.

Pamoja na kuidakia KMC, lakini anaitumikia timu ya taifa, Taifa Stars.

Yeye amesimama langoni mara 11 bila kuruhusu wavu wake.

**7. Aron Kalambo-Dodoma Jiji**

Ni mmoja kati ya makipa wenye uzoefu mkubwa kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara, akiwa pia ameshawahi kuzidakia Mbeya City, Prisons na sasa Dodoma Jiji.

Msimu huu tayari ana 'clean sheets' 11 kama Kaseja na kuwa mmoja wa makipa bora msimu huu.

**8. Daniel Mgore-Biashara United**

Mmoja wa makipa vijana kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara. Tangu msimu uliopita amekuwa akihusishwa kuihama klabu yake ya Biashara United, lakini anabaki.

Amesimama langoni bila kuruhusu bao mara 10, akiunda orodha ya makipa wa Kibongo bora kabisa msimu huu ambao wamepata 'clean sheets' nyingi kwenye Ligi Kuu.

## JE, WAJUA?



ARGENTINA imebeba kwa mara ya kwanza kombe la Copa America tangu mwaka 1993, na hivyo hivyo wamemaliza ukame wa miaka 28, baada ya kuifunga Brazil bao 1-0 kwenye fainali iliyopigwa Jumamosi usiku.



## HABARI DODOMA

# Walimu wakatazwa vijiwe vya bodaboda

Na Renatha Msungu, DODOMA

TUME ya Utumishi wa Walimu (TSC) imewataka wahitimu wa Ndaki ya Ualimu wa Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM)

kwenda kufanya kazi ya taaluma yao badala ya kuwa madereva wa bodaboda katika vijiwe.

Aidha, Chama cha Walimu Tanzania CWT kimewaagiza walimu kwenda kusimamia maadili ya kazi yao ili kuendelea kuipa serikali imani katika kusimamia mitihani ya kitaifa badala ya Jeshi la Polisi.

Hayo, yalisemwa na Mkurugenzi Msaidizi Ajira na Maendeleo ya Walimu kutoka TSC, Mectildis Kapinga, wakati wa kongamano la Mwalimu wa Karne ya 21, lililokwenda sambamba na kuwaaga wahitimu wa kada ya ualimu UDOM.

Kapinga alisema unakuta mwalimu badala ya kwenda kujitolea kufundisha katika shule mbalimbali ili kuimarisha ujuzi alioupata chuoni, yeye anakwenda kupiga kambi katika vijiwe vya bodaboda.

"Naomba mtakapohitimu muende kufanya kazi mlioisomea na kuichagua, taifa linawahitaji," alisema Kapinga.

Alifafanua kuwa kuna misingi ya walimu inajengwa katika nguzo tano ambazo wanatakiwa kuzizingatia ili waweweze kusonga mbele katika kada hiyo.

Mbali na hilo, aliwataka wanapokwenda kufanya kazi hawapaswi kulewa madaraka badala yake wafanye kwa bidii na weledi ili kuipeleka mbele taaluma hiyo.

Alisema wanapaswa kutumia elimu walioipata vizuri kuwafundisha wanafunzi ikiwamo kuwa na utii na uaminifu mkubwa wanapokuwa kazini.

Katibu Mkuu wa CWT, ambaye alikuwa mgeni rasmi katika Kongamano hilo, Mwalimu Deus Seif, alisema wahitimu hao wanapaswa kuzingatia maadili ya taaluma hiyo ili serikali

iendelee kuipa imani sekta hiyo katika suala la usimamiaji mitihani ya taifa.

Seif, alisema umefika wakati sasa walimu wa karne ya 21 kuwa watii katika kazi ili waifanye kada ya ualimu kuwa bora na kuvutia machoni mwa jamii.

"Msiende kuwa watu wa kuhangaika mtaani, jitumeni katumieni Chama cha Walimu li muweze kusonga mbele," alisema Seif.

Vile vile, aliwasisitiza kuitumia Benki ya Mwalimu ili kujiwekea akiba yao ya baadaye kama walimu wa karne ya 21.

Seif alisema ufike wakati walimu tuchangamkie fursa zinazotolewa kwa ajili yao ambazo zitachangia kujiongezea kipato katika kada yao.




Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya - Idara ya Maendeleo ya Jamii, Patrick Golwike, akizungumza na viongozi kwenye mkutano wa Baraza la Taifa la mashirika yasiyo ya kiserikali (NACONGO) uliofanyika Dodoma juzi. **PICHA: PETER MKWAVIL**

# Serikali kuendeleza hamasa kwa wakulima

Na Renatha Msungu, DODOMA

SERIKALI imesema itaendelea kuweka hamasa kwa wakulima ili kuongeza uzalishaji wa mazao na kuwawezesha kulima kibiashara.

Hayo yalisemwa na Waziri wa Kilimo, Prof. Adolf Mkenda, wakati wa mazungumzo na Mkurugenzi Mkaazi wa Shirika la Misaada la Kimataifa la Marekani (USAID), Andy Karas.

Katika mazungumzo hayo Prof. Mkenda alimweleza Mkurugenzi huyo kuwa Wizara ya Kilimo imejipanga kufanya mageuzi makubwa katika sekta hiyo ili kuondokana na dhana ya kilimo cha kujikimu na kuhamia katika kilimo cha kibiashara. Waziri Mkenda, alisema kuwa ili kuongeza tija katika kilimo, serikali imejipanga kuimarisha utafiti katika mazao mbalimbali ya kibiashara na chakula.

Hata hivyo, alisema kuwa maendeleo ya kilimo yanategemea zaidi utafiti husussani wa udongo ili kujua kila eneo linapaswa kulimwa zao gani ili waweze kusonga mbele.

Alisema wizara imebaini teknolojia bora itakayopelekea kukisogeza kilimo katika hatua kubwa ya mafanikio na kimageuzi ili kuleta tija kwa wakulima.

Alisema pamoja na mambo mengine wizara pia imejipanga katika kuongeza thamani ya mazao ya kilimo kuliko kusafirisha bila kuongeza thamani.

"Tukiongeza thamani ni wazi kuwa uchumi utapanda, lakini zaidi ajira zitaongezeka kwa wananchi, tutakuwa na pato zuri la kigeni sambamba na utambulisho wa nchi," alisema Prof. Mkenda.

Kuhusu sekta ya umwagiliaji Waziri Mkenda alisema Tanzania ina jumla ya hekta zaidi ya milioni 29, zinazofaa katika umwagiliaji, lakini ni hekta zisizofikia milioni moja ndizo ambazo zimefanyiwa kazi.

"Kwa maana hiyo kuna fursa kubwa katika umwagiliaji, hivyo ninyi kama wadau kadhalika natoa wito kwa wadau wengine kujitokeza kuwekeza katika umwagiliaji," alisema Prof. Mkenda.

Karas aliipongeza serikali kwa mikakati madhubuti ya kuimarisha sekta ya kilimo.

# Azaki zaomba kikao na Samia

Na Paul Mabeja, DODOMA

BARAZA la Taifa la Mashirika yasiyo ya Kiserikali (NACONGO) limemwomba Rais Samia Suluhu Hassan, kukutana nao na kuzungumza kuhusu mustakabali wa NGOs kwa maendeleo ya taifa.

Mwenyekiti wa Baraza hilo, Lilian Badi, alitoa ombi hilo mbele ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Dk. Dorothy Gwajima, wakati akizindua rasmi Baraza la NACONGO.

Badi alisema kuwa lengo la kutaka kukutana na Rais Samia, ni kuweka mwelekeo mzuri kwa mashirika yasiyo ya kiserikali katika jitihada za kuhakikisha yanasaidiana na kuwaletea maendeleo wananchi katika utekelezaji wa miradi mbalimbali.

Aliongeza kuwa Baraza hilo litahakikisha linaleta umoja kati ya mashirika yasiyo ya kiserikali nchini, wadau na serikali ili kuhakikisha inasaidia utekelezaji wa mipango mikakati iliyowekwa na katika kuwaletea wananchi maendeleo.

Akizungumza kwa niaba ya serikali Kaimu Katibu Mkuu Wizara ya Afya-Idara Kuu ya Maendeleo ya Jamii, Patrick Golwike, alilitaka baraza hilo kufanya kazi kwa kuzingatia sheria, taratibu na tamaduni za nchi ili kusaidiana na serikali katika kutatua changamoto zinazowakabili wananchi katika kujiletea maendeleo.

Kadhalika, alisema kuwa baraza hilo linatakiwa kuhakikisha linaweka maslahi ya taifa mbele na kuhakikisha linasimama kwa niaba ya mashirika yote na sio kwa ajili ya machache tu.

Mwenyekiti wa Bodi ya Uratibu wa mashirika yasiyo ya kiserikali, Dk. Richard Sambaiga, alilipongeza baraza hilo kwa kuchagua viongozi wake na kuwataka kuwa jicho kwa mashirika yasiyo ya kiserikali nchini.

Hivi karibuni Waziri Gwajima aliunda kamati ya uratibu wa uchaguzi wa NACONGO kufanikisha uchaguzi wa viongozi wa baraza hili kuanzia ngazi ya wilaya hadi taifa.





Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi Maryprisca Mahundi, akifungua maji ya bomba katika Kijiji cha Kanganga, Kata ya Mawindi, wilayani Mbarali baada ya mradi huo kuwa katika hatua za kukamilika na kuanza kukinufaisha kijiji kimoja kati ya sita vya kata hiyo. Kulia ni Mkuu wa Wilaya, Reuben Mfune. **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# Wakazi Mjele kupata maji ya bomba

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

WANANCHI wa Kata ya Mjele, iliyoko Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, wanatarajiwa kupata huduma ya maji ya bomba baada ya Wizara ya Maji kupitia Wakala wa Majisafi na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), kukamilisha mradi wa maji ambao utaanza kuwahudumia wananchi wa eneo hilo ifikapo mwezi Septemba, mwaka huu.

Naibu Waziri wa Maji, Mhandisi, Maryprisca Mahundi, alitoa kauli hiyo jana alipotembelea mradi huo Kata ya Mjele na kuwahakikishia wananchi kuanza kunufaika na maji ya bomba baada ya miundombinu mingine ya mradi huo kukamilika, Septemba, mwaka huu.

Alisema mradi huo hadi kukamilika, utagharimu Sh. bilioni mbili na tayari RUWASA wanaendelea na ujenzi wa miundombinu kwenye maeneo mbalimbali ya wananchi ili kuhakikisha maji ya bomba yanapatikana kwenye maeneo yao.

"Katika kuhakikisha mradi huu unakamilika kwa muda uliopangwa mwisho wa mwezi wa saba, wizara itawapatia kiasi cha fedha Sh. milioni 500 kwa ajili ya ununuzi wa mabomba licha ya Meneja wa RUWASA kusema mradi huo utakamilika baada ya miezi sita, lakini niombe kufika mwezi wa tisa baadhi ya meneo ikiwamo Mjela ambao wako karibu na mradi huu waanze kupata maji," alisema Mhandisi Mahundi.

Diwani wa Kata ya Mjele, Tatizo Julius, alisema adha ya maji katika kata hiyo inasababisha wanawake kununua kwa Sh. 1,000 kwa ndoo kiasi ambacho ni kikubwa kulinganisha na uchumi wa kipato chao.

Alisema kata hiyo imetaabika na adha ya maji kwa miaka mingi na hulazimika kushirikiana na wanyama kipindi cha kiangazi maji ambayo sio safi wala salama.

Walisema wanashauku kubwa ya kutumia majisafi ya bomba na wako tayari kushirikiana na RUWASA kutoa nguvu kazi zao ili mradi huo ukamilike haraka.

Walisema kinamama wanatumia umbali wa kilomita 20 hadi 30 kufuata maji maeneo mengine na kuwakwamisha kwenye shughuli za uzalishaji.

Meneja wa RUWASA, Mkoa wa Mbeya, Hans Patrick alisema, mradi huo wa Mshewe-Mjele, unatarajia kukamilika baada ya miezi sita na utahudumia vijiji vinne vilivyopo Kata ya Mshewe.

# UWT Mbeya yawaonya wanaomchokonoa Mahundi

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

UMOJA wa Wanawake wa Chama Cha Mapinduzi (UWT) Mkoa wa Mbeya, wameapa kushughulika na mwanaCCM anayemnenea vibaya Mbunge wa Viti Maalum mkoani Mbeya, Mhandisi Maryprisca Mahundi, ambaye ni Naibu Waziri wa Maji.

Akizungumza jana wakati wa Baraza Maalum la UWT, Mwenyekiti wa Umoja huo, Oliva Kibona alisema atakayemchokoza mbunge huo atakuwa anaichokoza mboni ya jicho ya Mkoa wa Mbeya.

Alisema mbunge huyo amekuwa kiungo muhimu kwa maendeleo ya wanawake kwa sababu amewawezesha kiuchumi kwa kuwapitia fedha kila wilaya Sh. milioni 20 kwa ajili ya kuanzisha miradi, aliwapatia mitungi ya gesi ili kuepukana na matumizi ya kuni, vitenge vinavyoonyesha kuunga mkono jitihada za Rais Samia Suluhu Hassan pamoja na kila mwana umoja huo Sh. 10,000 ili kukimu mahitaji yake.

"Mahundi ametusaidia kurahisisha siasa za Mbeya tunatembea kifua mbele hakuna haja ya kutumia nguvu kwenye kampeni zijazo maana mambo makubwa aliyoyafanya bila kujali makundi ya kisiasa, nawaomba tumuunge mkono mwenzetu tuachane na chuki na visasi visivyokuwa na maana," alisema Oliva.

Kwa upande wake Mhandisi Mahundi alisema kupitia Taasisi yake ya Maryprisca Women Empowerment Foundation (MWEF), malengo yake ni kuwawezesha wanawake kiuchumi pamoja na kuboresha malezi na makuzi ya watoto wa kike ili kutimiza ndoto zao za kupata elimu na uongozi.

Kupitia shirika hilo atahakikisha wanawajengea uwezo wanawake katika masuala ya ujasiriamali na biashara ili waweze kujikimu kiuchumi, kuwawezesha wanawake kufaidika na fursa mbalimbali zinazojitokeza.

# Wadau waombwa kuendelea kutoa misaada

**Na Grace Mwakalinga,** KYELA

SERIKALI ya Wilaya ya Kyela imewaomba wadau na taasisi mbalimbali kuendelea kutoa msaada wa hali na mali kwa watoto yatima ili nao waishi kwa furaha.

Kauli hiyo ilitolewa jana na Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kyela, Ezekiel Magehema, wakati akipokea msaada wa mahitaji mbalimbali kwa ajili ya kuwasaidia watoto yatima.

Alisema mtu yeyote au taasisi yenye uwezo ni vyema ikajitoa kwa ajili ya kuwasaidia watoto wenye mahitaji katika jamii badala ya kutumia fedha kwenye mambo ya anasa.

Alisema kutoa msaada kwa watu wenye mahitaji kuna thawabu kubwa kwa Mwenyezi Mungu na kila mwenye uwezo aguswe na kutoa sadaka kwa watoto yatima ili abarikiwe.

Msaada wa vitu mbalimbali kama vile madaftari, mafuta ya kupaka, wenye thamani ya shilingi milioni moja ulitolewa na Mkurugenzi wa Asante Mbeya Project, Daniel Mwanakatwe kwa kushirikiana na wadau.

"Hawa watoto hawakupenda kuwa yatima bali ni mapenzi ya Mungu, mimi nimepita kwenye maisha magumu sana nilikuwa machinga barabarani natembeza bidhaa kwa mguu hapa wilayani Kyela sikukata tamaa sasa ni miongoni mwa vijana ambao wamepiga hatua hivyo nina sababu ya kurudisha shukurani kwa Mungu kupitia sadaka hii kwa watoto yatima," alisema Mwanakatwe.

Akipokea msaada huo kwa niaba ya watoto, Mbunge wa Jimbo la Kyela, Ally Jumbe, alisema wadau hao wamemsaidia mbunge huyo sehemu ya jukumu lake kuwahudumia wananchi na kwamba wamempa deni Mungu kwa kuwa shukrani na maombi ya watoto hao yataleta thawabu. Baadhi ya wafanyabiashara kutoka jijini Mbeya walioungana na Mwanakatwe kutoa msaada huo, walisema wamefurahishwa na wazo lake kuwasaidia watoto yatima kwa kuwa ni jambo lenye baraka.







Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Joyce Ndalichako, akiongea na wanafunzi na viongozi wa Taasisi ya Elimu ya Sayansi za Baharini ya Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Zanzibar akiwa katika ziara ya kikazi jana. **PICHA: MARTIN KABEMBA**

# Waziri ataka ushirikiano sekta ya elimu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Simai Mohammed Said, amesema kushirikiana katika utendaji wa kazi kutasaidia kufikia malengo katika kuendeleza sekta ya elimu nchini.

Akizungumza wakati wa kikao cha mashirikiano baina ya watendaji wa wizara ya Elimu Zanzibar na Tanzania Bara, katika ukumbi wa Taasisi ya Utalii ya Chuo Kikuu cha Taifa cha Zanzibar (SUZA), Maruhubi Mjini Unguja, alisema kushirikiana ni njia pekee ya kutatua changamoto zinazoikabili sekta ya elimu kwa Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Aliwataka watendaji wa pande mbili hizo kuhakikisha katika majadiliano yao wanazungumza kwa kuweka mikakati ya kutatua matatizo mbalimbali ya Muungano kupitia sekta ya elimu ili kuleta faida.

Alisema elimu ni sekta mama katika kuleta maendeleo kwenye kila taifa na kunahitaji mtazamo wa hali ya juu kuondoa changamoto zikiwamo vitabu, walimu mahiri pamoja na mambo yote yanayohusu sekta hiyo. Akizungumzia somo la dini kutokuwa na sifa ya kuongeza alama za ufaulu wa kujiunga na chuo, Simai aliwataka kuhakikisha wanajadiliana kwa kukiwekea mazingira rafiki kwa kuliingiza somo hilo ili kuondoa utata uliojitokeza.

Aliwasihi watendaji hao kushirikiana kwa kila namna hasa wakurugenzi na wakuu wa vitengo ili kuhakikisha mafanikio ya elimu yanapatikana kwa pande zote mbili za Muungano wa Tanzania.

Kwa upande wake Katibu Mkuu Wizara ya Elimu Tanzania Bara, Dk. Leonard Akwilapo, alisema ameshukuru kuendelea kufanyika mikutano kama hiyo ya ushirikiano baina ya wizara hizo mbili ambayo italeta mafanikio makubwa katika ukuaji wa elimu nchini.

Akiwasilisha ripoti ya mradi wa kuboresha elimu ya juu katika mageuzi ya uchumi (HEET), Kaimu Mkurugenzi wa Elimu ya Juu Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia Tanzania, Dk. Kenedy Hosea, alisema mradi huo umeshirikisha vyuo 19 vya Tanzania bara na visiwani.

Alisema pamoja na malengo hayo pia utalenga katika kubadilisha mitaala yenye tija kwa kuzingatia soko la ajira na umepangiwa bajeti ya dola milioni 425.

Kupitia mradi huo, Naibu Makamu Mkuu wa SUZA anayeshughulikia taaluma, Dk. Ali Makame Ussi, alisema chuo hicho kimejipanga kujenga majengo makubwa ikiwamo shule ya kilimo pamoja na maabara yake na maabara ya kufundishia Sayansi na maabara ya kompyuta na ofisi za wafanyakazi.

Kikao hicho cha ushirikiano kati ya watendaji wa wizara hizo mbili kimefanyika chini ya Mwenyekiti Katibu Mkuu Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar, Ali Khamis Juma, ambacho hufanyika kila mwaka.

# Rais Mwinyi afanya uteuzi Makatibu Wakuu, Manaibu

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dk. Hussein Ali Mwinyi, amefanya uteuzi wa Makatibu Wakuu na Manaibu Makatibu Wakuu.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi, Mhandisi Zena Ahmed Said, walioteuliwa ni Mussa Haji Ali kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais Ikulu na Habiba Hassan Omar ameteuliwa kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji.

Wingine ni Issa Mahfoudh Haji, aliyeteuliwa kuwa Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Aboud Hasssan Mwinyi, ameteuliwa kuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango, anayeshughulikia (Fedha na Mipango), kabla ya uteuzi huo alikuwa Mkuu wa Wilaya ya Kaskazini B Unguja.

Pia amemteua Mikidadi Mbarouk Mzee, kuwa Naibu Katibu Mkuu, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ. Uteuzi huo umeanza Julai 10, 2021.

Aidha wateuliwa wote waliotajwa wataapishwa leo saa 4.00 asubuhi Ikulu Zanzibar.

# Wabunge, Wawakilishi waonywa migogoro

**Na Mwandishi Wetu**

NAIBU Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) Zanzibar, Dk. Abdulla Juma Mabodi, amewataka baadhi ya wabunge, wawakilishi na madiwani wanaogombana na kuendeleza migogoro katika majimbo yao kuacha tabia hiyo.

Angalizo hilo alilitoa katika ziara yake ya kukagua utekelezaji wa ilani na kuimarisha uhai wa chama katika maeneo mbalimbali ya Mkoa wa Kusini Unguja.

Alisema viongozi wana jukumu la kuwatumikia wananchi na hawana sababu ya kutofautiana na kuanzisha migogoro isiyokuwa ya lazima katika maeneo yao.

Alisema kuna baadhi ya viongozi wa majimbo nchini wamekuwa na migogoro ya kugombana wenyewe kwa wenyewe badala ya kuwatumia wananchi hali inayokwamisha maendeleo ya majimbo hayo.

Alitoa onyo kali kwa kueleza kwamba CCM haiwezi kuwavumilia viongozi wa aina hiyo na haitosita kuchukua hatua kali za kinidhamu dhidi yao kwa kuwa waliomba ridhaa ya uongozi huo kwa uamuzi wao bila kulazimishwa.

"Kupitia maelekezo ya vikao vikubwa vya Kamati Kuu ya CCM Taifa tumeelekezwa tuwakumbushe viongozi wote wa ngazi mbalimbali wakiwamo wabunge, wawakilishi na madiwani kushuka kwa wananchi kusikiliza hoja, ushauri na changamoto zao kisha kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu," alisema.

Dk. Mabodi, aliwapongea wabunge na wawakilishi wa majimbo ya mkoa huo kwa juhudi zao za kuwatumikia wananchi na utekelezaji mzuri wa Ilani ya CCM katika maeneo mbalimbali majimboni mwao.

Dk. Mabodi, alisema lengo la ziara hiyo ni kukutana na mabalozi wa mashina ya CCM kubadilishana nao mawazo na kusikiliza hoja zao kwa lengo la kuzitafutia ufumbuzi wa kudumu.

Akizungumza kwa nyakati tofauti na mabalozi hao aliwaambia kwamba CCM inathamini uwepo wao kwani ndani ya Katiba ya CCM ya mwaka 1977 imetaja kuwa wao ndiyo wanachama namba moja. Kupitia ziara hiyo Dk. Mabodi, aliwasisitiza mabalozi hao kuendelea kufanya vikao vya kikatiba ili kujua mwenendo wa jamii husika pamoja na kujadili masuala mbalimbali ya kimaendeleo katika maeneo yao.

Alisema ushindi wa Chama katika uchaguzi mkuu wa 2020, umetokana na juhudi kubwa za kiutendaji zilizofanywa na mabalozi wa mashina katika maeneo mbalimbali nchini.

Kadhalika, alisema utamaduni wa kuonana na wanachama wa mashina na matawi kila ikikaribia uchaguzi umekwisha, badala yake Chama kimewaagiza viongozi wa ngazi zote wakiwamo Wabunge na Wawakilishi kushuka kwa wananchi kusikiliza hoja zao na kutafuta ufumbuzi.

## Mkemia Mkuu awazawadia wanafunzi bora kidato 4, 6

**Na Mary Geofrey**

MAMLAKA ya Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali (GCLA), imetoa zawadi kwa wanafunzi bora 36 wa kidato cha sita na cha nne waliofanya vizuri katika masomo ya Kemia, Fizikia na Bailojia pamoja na walimu sita waliofanya vizuri.

Zawadi hizo zilitolewa mwishoni wa wiki, Dar es Salaam na Mkemia Mkuu wa Serikali Dk. Fidelice Mafumiko, kwa lengo la kuinua ari ya wanafunzi kupenda masomo ya sayansi.

Alisema tangu kuanza kwa utaratibu wa kutoa zawadi kwa wanafunzi waliofanya vizuri katika masomo ya Sayansi miaka 14 iliyopita, ushindani umekuwa ukiongozeka kati ya shule, walimu na wanafunzi.

"Hali hii imeongeza kasi ya ufaulu wa wanafunzi wa masomo ya sayansi nchini na leo tunatoa tena zawadi kwa wanafunzi 36 wa shule mbalimbali za sekondari na walimu sita," alisisitiza Dk. Mafumiko.

Alisema anaamini jitihada na ari za wanafunzi ndio zimewafanikisha kuwa wanafunzi bora wa masomo ya sayansi.

Alitaja baadhi ya shule zilizotoa wanafunzi hao kuwa ni Canosa, Mzumbe, Feza Boys na Girls, St. Francis, St. Mary's Mazinde Juu, Msalato na Tabora Boy's.

Alisema kwa upande wa zawadi wameongeza kiwango kutoka Sh. 500,000 mwaka jana hadi 700,000 mwaka huu kwa wanafunzi wa kidato cha sita na kutoka Sh. 450,000 hadi Sh. 500,000 kwa kidato cha nne.

Dk. Mafumiko alitaja baadhi ya zawadi walizotoa kwa wanafunzi hao kuwa ni cheti pamoja na fedha taslimu Sh. 700,000 kwa nafasi ya kwanza kwa kila mmoja, Sh. 650,000 wa pili na Sh. 600,000 kwa nafasi ya tatu kwa wnaafunzi wa kidato cha sita.

Alieleza kuwa mwanafunzi wa kwanza wa kidato cha nne alipatiwa fedha taslimu Sh. 550,000, wa pili Sh. 500,000 na wa tatu Sh. 450,000.

Mwakilishi wa wanafunzi hao, Mwesiga Rwegerera, aliishukuru GCLA kwa zawadi walizotoa na kwamba zinawafanya kuendelea kujituma kusoma kwa bidii.

# NIT kunoa wahandisi wa ndege za Airbus

**Na Mwandishi Wetu**

WAKATI Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) kimefundisha wahandisi wa matengenezo ya ndege takribani 75 toka kilipoanza kutoa kozi hiyo mwaka 2015, sasa kimekubaliana na Kampuni ya Ndege ya Airbus kuwa kituo kwa Afrika kwa ajili ya kufundishia wahandisi wake.

Akizungumza baada ya kupokea vifaa vya kufundishia wanafunzi wa uhandisi wa matengenezo ya ndege kama ruzuku kutoka serikalini kupitia Mamlaka ya Elimu Tanzania (TEA), katika kampasi ya Chuo - Mabibo jijini Dar es Salaam, Mkuu wa NIT, Prof. Mganilwa, alisema

kitakuwa kituo cha Airbus kwa Afrika nzima katika kufundishia wahandisi wa ndege hizo, na tunategemea kuongea na kampuni nyingine ya ndege za Boeing na wenyewe tuweze kuingia nao ushirikiano katika kutoa mafunzo.

Alisema takribani wanafunzi 75 wameshafuzu mafunzo ya uhandisi wa matengenezo ya ndege toka walipoanza ramsi kutoa kozi hii mwaka 2015, ambapo wanafunzi 49 walifuzu katika shahada ya kwanza na 26 walifuzu astashahada.

Prof. Mganilwa aliongezea: "Kozi hii ya uhandisi wa matengenezo ya ndege inatolewa nje ya nchi kwa ada ya takribani milioni 200 hadi milioni 300, lakini katika chuo chetu mwanafunzi wa kozi hii anasoma kwa ada ya shilingi milioni 6 kwa mwaka."

"Tunataka kuondoa tofauti kubwa iliyopo ya wahandisi wa nje waliopo nchini, ambao ni asilimia zaidi ya 60, kwa kuhakikisha tunazalisha wahandisi wengi wazawa wa matengenezo ya ndege," alisema.

Profesa Mganilwa ameiomba serikali kwamba pamoja na mkopo unaotolewa kwa wanafunzi wa shahada ya kwanza ambao ni asilimia 51.7, ifikilie kuwasaidia kama msaada kwa asilimia 48.3 inayobaki ambayo wanatakiwa walipe wao wenyewe, hii ni kutokana na wengi wao kutoweza kulipa ongezeko hilo kwa wakati.

Naye Mkurugenzi wa TEA, Bahati Geuzye, alisema vifaa vilivyokabidhiwa kwa NIT ni kwa ajili ya mafunzo kwa vitendo kwa wanafunzi wa kozi za uhandisi wa matengenezo ya ndege vinagharimu kiasi cha shilingi milioni 245.4.

"Vifaa hivi ni mojawapo ya ruzuku kutoka serikalini inayosimamiwa na TET lengo likiwa ni kuboresha mafunzo ya uhandisi wa matengenezo ya ndege kwa vitendo katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji kwenye eneo la usafiri wa anga," alisema.

Akizungumza kabla ya kukabidhi vifaa hivyo, Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Prof. Joyce Ndalichako alikipongeza chuo

kwa kuwa mfano wa vyuo vya kimkakati katika kufundisha mafunzo yanayoakisi dira ya serikali ya Rais Samia Suluhu Hassan.

"Serikali inahitaji kuona vyuo vya elimu ya juu vikitoa kozi ambazo zinakwenda sambamba na mipango ya serikali ili kufanikisha kufikia malengo yaliyowekwa," alisema.



Waziri wa Elimu, Sayansi, Teknolojia na Ufundi, Prof. Joyce Ndalichako akiwa na Mkuu wa Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT), Prof. Zacharia Mganilwa, wanafunzi wa uhandisi wa ndege na wahudumu wa ndege, baada ya kukabidhi vifaa vya kufundishia kama ruzuku kutoka serikalini jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **MPIGAPICHA WETU**

# Wajasiriamali wanaochipukia wakutanishwa kukabili vikwazo

**Na Mwandishi Wetu**

CHANGAMOTO ya urasimishwaji wa biashara miongoni mwa wajasiriamali na wafanyabiashara wanaochipukia imetajwa kuwa moja ya kikwazo kikubwa kwa wao kuendesha shughuli zao kwa ushindani na hivyo kukosa ukuaji endelevu.

Katika kukabiliana na changamoto hiyo, Mamlaka ya Biashara Tanzania (TANTRADE) kwa kushirikiana na Benki ya NBC pamoja na taasisi nyingine 15 zimeweka kambi kwenye Maonyesho ya 45 ya Kimataifa ya Biashara ya jijini Dares Salaam 'Sabasaba' ili kuwasaidia wafanyabiashara hao.

Akizungumza kwenye maonyesho hayo mwishoni mwa wiki, Ofisa Habari Biashara wa TANTRADE, Miriamu Kikoti, alisema kupitia Kliniki ya Biashara inayosimamiwa na TANTRADE na kudhaminiwa na Benki ya NBC wameweza kuwakutanisha wataalamu wa Biashara kutoka taasisi mbalimbali za umma na binafsi ambao hushirikiana katika kutatua changamoto mbalimbali zinazowakabili wajasiriamali na wafanyabiashara nchini ikiwamo suala zima la urasimishwaji biashara.

Kikoti alizitaja taasisi nyingine zinazoshiriki kikamilifu kufanikisha mkakati huo wa pamoja ni EPZA, BRELA, TIC, GS1, TRA, WMA, TBS, SIDO, FFC,UDSM,TIRA,TFS, GCLA, FCC, TMDA na OSHA.

"Changamoto kubwa kwao ni urasimishwaji wa biashara zao. Hadi kufikia sasa mbali na kutoa huduma za ushauri kwa mamia ya wajasiriamali na wafanyabiashara wanaochipukia wanaotutembelea kila siku tangu maonesho haya yaanze, tumefanikiwa kuwasaidia wajasiliamali zaidi ya 120 kuelekea katika urasimishwaji wa biashara zao."

"Hili tunalifanya kwa urahisi sana kwa sababu kupitia kliniki hii wahusika wanapata cheni iliyokamilika na hivyo wanaondoka wakiwa wamekalimisha kila kinachohitajika," alifafanua.

Aliishukuru Benki ya NBC kwa kudhamini kliniki hiyo kwa kuwa mkakati huo mbali na kuwasaidia wajasiriamali hao, kwa kiasi kikubwa pia umekuwa ukifungua njia kwa taasisi za kifedha kutoa huduma za mikopo kwa wajasiriamali ambao wana sifa za kukopesheka kutokana na kuendesha shughuli zao kwa urasmi unaotakiwa na taasisi hizo huku pia wakiwa na uhakika wa kufanya marejesho ya mikopo.

Mafanikio ya kliniki hiyo yalidhihirishwa Oktoba 14, 2020 ambapo ilitajwa kuwa mshindi wa tatu wa dunia (Best use of partnership category) na wa pekee kutoka nchi za Afrika kwenye Tuzo za Taasisi zinazosimamia Biashara duniani (WTPO Awards 2020)

Mkuu wa Chapa na Mawasiliano kutoka NBC, David Raymond, alisema kwa kutambua umuhimu wa urasimishwaji biashara miongoni mwa wajasiriamali na wafanyabiashara wanaochipukia nchini benki hiyo haikusita kufadhili kliniki hiyo ili kuyaandaa makundi hayo yaweze kupata vigezo vitakayoyawesha kupata huduma mbalimbali za benki hiyo ikiwamo mikopo.

Alitolea mfano akaunti ya 'NBC Kua Nasi' inayowalenga wafanyabiashara wanaochipukia wakiwamo mamalishe, madereva bodaboda, wasindikaji, wasusi pamoja na makundi mengine kwa kuwawezesha kutunza pesa zao kwa usalama na urahisi zaidi bila gharama za uendeshaji.

HABARI KIMATAIFA

# Soko Kuu Mombasa lateketea kwa moto

**Mombasa, KENYA**

SOKO maarufu la Marikiti mjini Mombasa, limepata hasara kubwa kutokana na moto ambao ulilikumba soko hilo juzi, usiku wa kuamkia Jumapili.

Wafanyabiashara katika soko hilo, mjini Mombasa wamepata hasara kubwa baada ya moto mkubwa kushuhudiwa Jumamosi.

Hakuna ripoti za maafa wala majeruhi kufikia sasa huku juhudi za kuzima moto huo zikiendelea.

Magari ya zimamoto kutoka kitengo cha serikali za ugatuzi wakishirikiana na polisi wako kwenye tukio wakijaribu kudhibiti hali hiyo.

Wakati huu kukiwa na sharti la kutotoka nje usiku kwa sababu ya kuzuia maambukizi ya virusi vya corona, baadhi ya wakazi wa maeneo ya karibu wako nje, kushuhudia moto huo na wengine wakitoa msaada wa kudhibiti moto.

Hali hiyo, imewalazimu maofisa wa kushika doria nyakati hizo kuweka usalama eneo hilo pia kuepusha visa vya uporaji kutokea kwenye baadhi ya maduka yaliyoachwa wazi kutokana na moto huo.

Haijabainika chanzo cha moto huo.

*VOA*



Martine Moïse, mjane wa Rais wa Haiti Jovenel Moïse, enzi za uhai wa mume wake. Martine ameelezea jinsi alivyoshuhudia mume wake akimiminiwa risasi na wauaji bila kumpa dakika chache kujitetea. **PICHA: BBC**

# 'Mume wangu hakupata hata dakika 1 kutoa neno la mwisho'

**Port-au-Prince, HAITI**

MJANE wa aliyekuwa wa rais wa Haiti, Martine Moïse ameeleza namna wauaji walivyommiminia risasi mumewe baada ya kuingia nyumbani kwao usiku.

"Ghafla, mamluki waliingia nyumbani kwangu na kumuua mume wangu kwa risasi, kitendo hiki hakina jina kwa sababu lazima uwe mhalifu sugu kumuua rais kama Jovenel Moïse, bila hata kumpa nafasi ya kusema neno moja."

Martine Moïse amesema shambulio hilo lilitokea kwa muda mfupi sana na mumewe Jovenel, hakuweza kusema hata neno moja.

Rais Moïse aliuawa Julai 7, mwaka huu ikidaiwa na mamluki 28 wa kigeni kutekeleza tukio hilo.

Martine pia alijeruhiwa katika shambulio hilo na alisafirishwa kwenda Miami, Marekani kwa matibabu.

Jumamosi, alitoa ujumbe wa sauti kwenye ukurasa wake wa Twitter, akiapa kuendelea na kazi yake.

Alidai kwamba mumewe alikuwa akilengwa kwa sababu za kisiasa, hasa akitaja kura ya maoni juu ya mabadiliko ya katiba ambayo ingeweza kumpa rais nguvu zaidi.

Watu hao ambao hawajulikani alisema, "wanataka kuua ndoto ya rais".

"Ninalia ni kweli, lakini hatuwezi kuiacha nchi ipotee. Hatuwezi kuruhusu damu ya Rais Jovenel Moïse, mume wangu, rais wetu ambaye tunampenda sana na ambaye alitupenda sisi, kupita bure."

Moïse mwenye umri wa miaka 53, alikuwa rais wa Haiti, taifa maskini zaidi katika Amerika, akiongoza tangu mwaka 2017.

Wakati wake ofisini ulikuwa mgumu, alikabiliwa na tuhuma za ufisadi na kulikuwa na maandamano mengi katika mji mkuu na miji mingine mapema mwaka huu.

Uchaguzi wa bunge, ulipaswa kufanywa Oktoba mwaka 2019, mizozo ilichelewesha, ikimaanisha Moïse alikuwa akitawala kwa amri.

Alikuwa amepanga kufanya kura ya maoni juu ya mabadiliko ya katiba yaliyopendekezwa Septemba mwaka huu.

Katiba inasema bunge linapaswa kuchagua rais mwingine. Ingawa mizozo ilimaanisha kuwa uchaguzi uliopangwa kufanyika Oktoba mwaka 2019 haukufanyika na Moïse alikuwa akitawala kwa amri wakati maandamano yalipoenea.

Marekebisho ya katiba ambayo hayakubaliwi na kila mtu yanaonyesha kuwa waziri mkuu ndiye anayepaswa kuchukua nafasi hiyo.

Haiti ina waziri mkuu wa muda, Claude Joseph na mteule mpya, Ariel Henry, ambaye bado hajaapishwa.

Ijumaa, kikundi cha vyama vya siasa kilitia saini azimio la kumtangaza rais mpya, Joseph Lambert na Henry akishikilia nafasi ya Waziri Mkuu wake.

Hatua hiyo haijafanya mengi kutatua machafuko ya kisiasa na kiuchumi ambayo kwa muda mrefu yamelizonga taifa hilo.

*BBC*

## Chama cha PP chashinda uchaguzi

**Addis Ababa, ETHIOPIA**

TUME ya Uchaguzi ya Ethiopia, imetangaza ushindi wa Chama cha PP ambao umemhakikishia Abiy Ahmed, muhula mwingine wa miaka mitano madarakani.

Chama cha Prosperity (PP) cha Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed, kimeshinda viti vingi katika uchaguzi wa bunge la Ethiopia.

Waziri Mkuu Abiy na chama chake kipya cha PP walitangazwa kushinda kwa kishindo na tume ya uchaguzi katika hafla iliyofanyika kwenye mji mkuu wa Ethiopia, Addis Ababa.

Abiy ameupongeza uchaguzi huo na raia wa Ethiopia walipiga kura Juni 21, mwaka huu.

Alisema huo ni uchaguzi wa kwanza huru na wa haki kufanyika baada ya miongo kadhaa ya utawala wa ukandamizaji.

Tume ya Uchaguzi ilitangaza kuwa Chama cha Abiy cha Prosperity (PP) kimeshinda viti 410 kati ya viti 436 vya bunge katika maeneo ya uchaguzi uliofanyika.

Upigaji kura haukufanyika katika maeneo ya bunge yote 547 ya nchi hiyo, kutokana na mgomo wa upande wa upinzani, vita katika mkoa wa Kaskazini wa Tigray, vurugu za kikabila na tatizo la kufikishwa vifaa vya kupigia kura kwenye maeneo matatu kati ya majimbo 10, Ethiopia.

Uchaguzi utafanyika Septemba 6 mwaka huu, katika maeneo ya Harar na Somali ingawa Jimbo la Tigray, bado halijapangiwa tarehe ya kufanyika uchaguzi.

Mwenyekiti wa Tume ya Uchaguzi Birtukan Mideksa, amekiri kuwapo matatizo na kusema mchakato wa kupiga kura umewahakikishia watu juu ya uwepo wa serikali walioichagua kupitia kura zao.

Wakati huo huo, Tume ya Uchaguzi ilisema uchaguzi utarudiwa kwenye maeneo 10.

Matokeo ya uchaguzi huo yameonyesha kwamba vyama vya upinzani Ethiopia na wagombea huru walipata idadi ndogo ya kura.

Katika ujumbe wake kwenye mtandao wa Twitter, Waziri Mkuu wa Ethiopia Abiy Ahmed, ameandika kuwa, uchaguzi huo ni wa kihistoria na kwamba chama chake kimepata faraja kubwa kwamba kimechaguliwa na watu kuiongoza nchi.

Uchaguzi huo wa Juni 21 ni wa kwanza kwa Abiy kupigiwa kura, tangu alipoteuliwa kuwa waziri mkuu mwaka 2018 baada ya maandamano ya miaka kadhaa yaliyopinga serikali.

*DW*



# BALE kuachana na soka 2022

**MADRID, Hispania**

NYOTA wa Real Madrid na timu ya Taifa ya Wales, Gareth Bale, atastaafu kucheza soka ngazi ya Klabu ifikapo Juni 2022, kwa mujibu wa BBC Sport.

Bale amerejea Madrid baada ya kumaliza msimu mmoja wa mkopo alipokuwa akicheza kule Tottenham Hotspur.

Kurejea kwa Bale Madrid ni sehemu ya kumalizia mkataba wake wa mwaka mmoja uliosalia hapo Santiago Bernabeu.

Akiwa anapokea mshahara wa pauni 600,000 kwa wiki, Bale anampango wa kuachana na soka la klabu pindi aatakapomaliza mkataba wake na Madrid.

Kwa mujibu wa ripoti hiyo, Bale ataipeperusha bendera ya Wales kama timu hiyo itafanikiwa kufuzu michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar.

Wales inapointi 3 baada ya michezo miwili kwenye hatua ya makundi na ili kufuzu kucheza Kombe la Dunia, inapaswa kumaliza kama vinara wa kundi au wamalize nafasi ya pili na watacheza kwenye kapu la mtoano.

Na iwapo Wales itashinda kufuzu mashindano ya Kombe la Dunia maana yake ni kwamba Bale ataonekana uwanjani kwa msimu mmoja pekee kabla ya mchezaji huyo kustaafu akiwa na umri wa miaka 32.

# Mfumo wa Euro 2020 kutotumika tena – Rais

**NYON, Uswisi**

BAADA ya michuano ya Euro 2020 kumalizaika kwa fainali iliyopigwa jana Jumalipi kati ya Italia na England, Rais wa shirikisho la Ulaya, Aleksander Čeferin amesema kuwa hawatorudia makosa ya mfumo mechi walioutumia safari hii.

Katika mazungumzo na kipindi kimoja cha televisheni, Ceferin mesema kuwa michuano ya mwaka huu imekuwa na mapungufu makubwa hasa kutokuwa na usawa. Hii inatokana na ukweli kuwa baadhi ya timu zililazimika kusafiri umbali mrefu zaidi ya nyingine.

Katika michuano ya Euro 2020, kulikuwa na zaidi ya miji 11 ambayo ilikuwa ikishuhudia timu 24 zikigombania nafasi ya kuwa bingwa wa nchi za Ulaya.

"Kwa namna moja naona sio vizuri. Haiwezekani timu moja isafiri kilometa 10,000 wakati nyingine isafiri kilometa 1,000. Ni wazo zuri lakini sidhani kama tutalifanya tena," alisema Ceferin katika mahojiano hayo.

Suala la kuwa na zaidi ya miji 11 katika kuandaa michuano hii ilikuwa ni kwa ajili ya kuzuia au msongamano mkubwa kutokana na hali ya sasa ya janga la virusi vya corona.




# Koeman hawezi kuondoka Barcelona




**BARCELONA, Hispania**

MSHAURI wa Barcelona, Jordi Cruyff amekataa mawazo kuwa klabu hiyo inaweza kupata mbadala wa Ronald Koeman.

Koeman alionekana kuwa mbioni kuondoka klabuni hapo, huku taarifa zingine zikibainisha kuwa rais Joan Laporta alimwambia kuwa anaweza kusalia ikiwa klabu itamkosa mbadala wake.

Suala hilo lilipelekea kushambuliwa kwa Barcelona mitandaoni, wakiambiwa kuwa hiyo haikuwa jambo sahihi kumfanyia Koeman, huku mawakala pia wakishikilia msimamo huo.

Na sasa mujibu wa Cruyff ambaye ni meneja Koeman amesema kuwa hawezi kubadilishwa.

Cruyff alirejea Barcelona kama mshauri wa kimkakati klabuni hapo na anaaminiwa kuwa na ushawishi mkubwa kwa klabu.

Nyota huyo wa zamani wa Barcelona amekataa kabisa kuwa wanaweza kumpata meneja mpya ambaye atakuwa mbadala wa Koeman.

"Sifikiri kabisa hilo, na pia siyo nia ya Barcelona kumbadilisha Koeman kwa sasa. Kwangu itakuwa ni kitu kibaya sana," alisema Cruff akinukuliwa na Marca.

## HABARI MICHEZO

# Deschamps kuendelea kuwa kocha Ufaransa

**PARIS, Ufaransa**

DIDIER Deschamps ataendelea kuwa kocha Mkuu wa timu ya taifa ya Ufaransa, rais wa Shirikisho la Soka la Ufaransa, amethibitisha.

Deschaamps alisimamia kampeni ya Euro 2020 wakati Ufaransa ilipotupwa nje katika hatua ya 16 ya mwisho na Uswizi.

Lakini, baada ya kuongoza Les Bleus kwenye kutwaa Kombe la Dunia mwaka 2018 na fainali ya Euro 2016 miaka miwili iliyopita, hatima yake inabaki na FFF.

Na alipoulizwa na Le Figaro kama Deschamps anastahili kubaki katika jukumu lake, Rais Noel Le Graet alitoa jibu la mkazo: "Jibu ni ndio.

"Nilipokea habari Jumatano huko Guingamp. Suala hilo lilitatuliwa kwa dakika tatu. Mapenzi yake yana nguvu sana kuendelea.

"Hakukuwa na mjadala juu ya," Tunafanya nini? Na, "Je! Tunafanyaje?"

Bosi wa Ufaransa tangu Julai 2012, Deschamps pia aliongoza nchi yake kutinga robo fainali ya Kombe la Dunia la 2014, ambapo badaye walichapwa na Ujerumani.

Ameshinda katika mechi 76 kati ya 117 alizocheza na timu ya taifa, akiipa ushindi wa asilimia 65.

Huo ni uwiano wa juu zaidi kwa mkufunzi yeyote ambaye amekuwa na angalau michezo 30 akisimamia Ufaransa.



# GUARDIOLA sasa amgeukia Griezmann




**MANCHESTER, England**

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amezungumza na mshambuliaji wa Barcelona, Antoine Griezmann juu ya uwezekano wa kuhamia Ligi Kuu ya England na kutua katika klabu hiyo.

Kwa mujibu wa jarida la FootMercato, Guardiola amezungumza moja kwa moja na mshambuliaji huyo katika wiki hii.

Barcelona ipo tayari kumuuza Griezmann kwani inataka kusawazisha bajeti katika masuala ya madeni wanayokabiliana nayo.

Hata hivyo, ni klabu chache zinazoweza kumudu kumnunua mshambuliaji huyo wa Ufaransa.

Kipaumbele cha Man City msimu huu wa joto ni Harry Kane, lakini kama Tottenham hawataki kushusha bei yao, Griezmann anaweza kuwa chaguo lao jipya.

Guardiola anaonekana kuwa shabiki wa Griezmann ambaye alitua pale Barcelona msimu uliopita na amekuwa hana kiwango cha kuvutia kama ilivyokuwa kule Atletico Madrid.



# Man United kuzipiku City, Chelsea kwa Kane

**LONDON, England**

KLABU ya Manchester United inaweza kuzipiku Manchester City na Chelsea kwenye mbio za kuwania saini ya Harry Kane, kwa mujibu wa Daily Mail.

Kocha wa Man City, Pep Guardiola, alisema wazi kuwa kutokana na gharama wanazotajiwa kwenye mchakato wa kusajili washambuliaji, kuna uwezekano mkubwa hatosajili mchezaji wa nafasi hiyo majira haya ya usajili wa kipindi cha majira ta joto.

Chelsea bado hawajafanya maamuzi kama wamsajili Kane au Erlind Haaland kutoka kule Borrusi Dortmund.

Hata hivyo, mahusiano yaliyopo kati ya Chelsea na Tottenham (mahasimu wa jiji la London) ni jambo lingine gumu kulikwepa.

Kwa mujibu wa Daily Mail, Man United wanaweza kukamilisha usajili wa Kane kama walivyofanya kwa Jadon Sancho waliyemnunua kwa pauni milioni 73.

Inasemakana yanayoendelea chini ya kapeti, yanawapa nguvu Man United kuliko City na The Blues hao.

Inasemekana Spurs wapo tayari kumwachia Kane kwenda United kama timu hiyo itatoa pauni milioni 100 na wachezaji wawili wa kikosi cha kwanza.

Ingawa haijawekwa wazi ni wachezaji gani wanaohusishwa na mchakato huo, lakini Man United wanauwezo wa kuwatoa baadhi ya wachezaji ili kumchukua Kane mwenye umri wa miaka 27.

## KWA UFUPI

### LORENZO AWANIWA

MANCHESTER United inalenga kufanikisha uhamisho wa pauni milioni 17 kumsajili beki wa kulia wa Napoli na Italia, Giovanni di Lorenzo baada ya mchezo wa mwisho wa jana Jumapili wa michuano ya Euro 2020 dhidi ya England. ***(Il Napolista, via Sun on Sunday)***

### TUCHEL NA HALAAND

KOCHA wa Chelsea, Thomas Tuchel klabu yake imsajili "haraka" mshambuliaji wa Norway, Erling Braut Haaland kutoka Borussia Dortmund. ***(Bild)***

### MAN NA KANE

MANCHESTER United haifanyi juhudi za kufikia makubaliano ya kubadilishana wachezaji ili kumleta mshambuliaji wa England, Harry Kane mwenye umri wa miaka 27 hapo Old Trafford kutoka Tottenham. ***(Sunday Express)***

### CAMAVINGA AWINDWA CHELSEA

CHELSEA imewasiliana na Rennes kuhusu uhamisho wa kiungo wa kati wa Ufaransa, Eduardo Camavinga mwenye umri wa miaka 18, ambaye anasakwa na Manchester United, Arsenal na Real Madrid. ***(Le Parisien - via Sun on Sunday)***

### AARONS AWANIWA EVERTON

KOCHA wa Everton, Rafael Benitez ana nia ya kusajili beki wa kulia na anamwangalia zaidi nyota wa Norwich City, Max Aarons mwenye umri wa miaka 21. ***(90mins)***

### PALMIERI ATAKIWA

NAPOLI watafanya kila wawezalo kumsajili beki wa Italia mwenye umri wa miaka 26, Emerson Palmieri kutoka Chelsea, ambapo, Kocha Luciano Spalletti amemtambua kipaumbele chake cha kwanza kipindi hiki cha usajili wa majira ya joto. ***(Corriere dello Sport)***

### ABRAHAM AGOMBEWA

KLABU ya West Ham wapo mstari wa mbele kutafuta sahihi ya mshambuliaji wa Chelsea, Tammy Abraham mwenye umri wa miaka 23, huku pia Aston Villa ikimwania nyota huyo. ***(Football Insider)***

### CORNET ATAKIWA BURNLEY

KLABU ya Burnley inawania kumsajili mlinzi wa Lyon, mwenye umri wa miaka 24, Maxwel Cornet, ambaye pia anasakwa na Hertha Berlin. ***(Sun on Sunday)***

### SPURS KUIPIKU MADRID

KLABU ya Tottenham inaweza kufanya iwe vigumu kwa Real Madrid kumsajili beki wa Ufaransa, Jules Kounde kutoka Sevilla. Spurs ipo tayari kutoa kiasi cha pauni milioni 51 kwa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 ambayo itakuwa zaidi ya ile inayotaka kutolewa na Madrid. ***(Sport)***

### ZIDANE AITAKA UFARANSA

KOCHA wa zamani wa Real Madrid, Zinedine Zidane mwenye umri wa miaka 49, hataki kurudi kufundisha klabu, badala yake anataka kuinoa timu ya taifa ya Ufaransa, inayonolewa na Didier Deschamps mwenye umri wa miaka 52. ***(L'Equipe - via ESPN)***

### BENZEMA KUBAKI MADRID

KARIM Benzema mwenye umri wa miaka 33, atasalia Real Madrid hata kama klabu hiyo ya Hispania itafanikiwa kumsajili Mfaransa mwenzake, Kylian Mbappe mwenye umri wa miaka 22 kutoka Paris St-Germain msimu huu wa majira ya joto.***(Marca)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# MESSI: NIMESUBIRI SANA KUBEBA TAJI NA ARGENTINA

●●●Kwake ni la kwanza, nchi hiyo imesubiri miaka 28 na sasa...

**RIO DE JANEIRO, Brazil**

LIONEL Messi ameelezea furaha yake na kutua mzigo mkubwa kwa kutwaa kombe na timu ya taifa ya Argentina, baada ya juzi Jumamosi usiku kubeba taji la Copa America 2021 kwa kuifunga Brazil kwenye dimba la Maracana.

Argentina iliibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Brazil baada ya Angel Di Maria kufunga bao dakika ya 22, na kumwezesha Messi ambaye ni mshindi mara sita wa Ballon d'Or kubeba taji na kikosi hicho cha La Albiceleste.

Messi na Argentina walimaliza nafasi ya pili kwenye Copa America mara tatu mwaka 2007, 2015 na 2016, pamoja na kuwa mshindi wa pili kwenye kombe la Dunia mwaka 2014 na ameelezea furaha yake.

"Nilihitaji kupata kitu fulani na timu ya taifa, nimekaribia mara nyingi sana kutwaa taji hli," aisema Messi akiwaambia waandishi wa habari.

"Nilijua kwamba kuna siku mambo yatakuwa sawa, itatokea na nafikiri huu ni wakati mzuri zaidi kuliko muda wowote.

"Nafikiri kwamba, Mungu aliuweka wakati huu kwa ajili yangu mimi, dhidi ya Brazil kwenye fainali na nchi yao."

Pamoja na Messi mwenye umri wa miaka 34 kutwaa taji hilo, pia ilikuwa ni mara ya kwanza kwa Argentina kubeba Copa America tangu mwaka 1993, hivyo wamemaliza ukame wa miaka 28.

"Bado hatuwezi kuamini kwamba sisi ni mabingwa kwa kile tulichofanikiwa kukitwaa," aliongeza Messi.

"Lakini nafikiri hii itakuwa mechi ya kumbukumbu kwenye historia ya maisha yangu, sio tu kwa sababu ni mabingwa wa Amerika Kusini, lakini kwa sababu tumewafunga Brazil kwenye nchi yao."

Argentina ilifikisha mechi 20 bila kufungwa chini ya kocha, Lionel Scaloni na imewapa nafasi nzuri kuelekea kwenye michuano ya Kombe la Dunia mwaka 2022 nchini Qatar.

Scaloni ameibadilisha Argentina, kwa kuwachezesha mara kwa mara nyota wapya, Emiliano Martinez, Rodrigo De Paul na Cristiano Romero ambao wamekuwa na kiwango cha kuvutia sana. "Lionel anastahili heshima hii," alisema Messi. "Mara zote ametaka kitu bora kwa timu ya taifa.

"Alijua kuwaweka watu pamoja na kwa hakika anastahili haki ya kutambuliwa kwa thamani yake."

HABARI MICHEZO

# WAANDAAJI FILAMU WALIA NA KODI ZA TRA

**Na Romana Mallya**

WAKATI Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ikizitaka kodi za waandaaji wa kazi za filamu, wenyewe wafunguka kuwa hukatwa zaidi ya mara tatu huku uandaaji wake ukitumia gharama kubwa.

Katika kikao kilichofanyika juzi mkoani Dar es Salaam baina ya TRA na waandaaji wa kazi za filamu, mamlaka hiyo ilisema kundi hilo lina wajibu wa kuchangia kodi pamoja na uwapo wa makato yanayotozwa maeneo ambako kazi hizo zinauzwa.

Akizungumza na kundi hilo, Naibu Kamishna Operesheni za Kodi, Swaleh Biyarugaba, alisema ulipaji wa kodi unamuhusu kila mfanyabiashara anayeingiza mapato kwa mwaka yanayoanzia Sh. milioni nne na kuendelea.

Kiongozi huyo alisema kikubwa ninachotakiwa ni kuendelea kuwapa elimu ili watambue wajibu huo.

"Producer 'mtayarishaji' wanaingiza fedha kupitia kazi wanazozifanya, anaweza kupewa shilingi milioni 200 hadi shilingi milioni 500 kwa kazi moja na hii ni kulingana na ukubwa wa kazi yenyewe, anapaswa kulipa kodi," alisema.

Rais wa Shirikisho la Filamu Tanzania (TAFF), Elia Mjata, alisema wamekutana na TRA kutokana na kuwapo kwa kilio cha muda mrefu kuhusu kodi ambazo wamekua wakikatwa waandaaji wa filamu.

Alisema wamekutana ili kuweza kupata elimu kuhusiana na kodi hizo na umuhimu wake katika ujenzi wa taifa.

Mwandaaji wa kazi za filamu, Jacob Steve maarufu JB, alitaka kwanza TRA ifuatilie namna kazi za filamu zinavyoandaliwa kabla ya kuwarundikia kodi.

"Ifike mahali TRA mje mjifunze kwetu namna tunavyozipika filamu, mfahamu tabu tunazopitia katika kuziandaa pamoja na gharama zilizopo," alisema.

Mwandaaji mwingine wa filamu wa siku nyingi, Jimmy Mafufu alisema kazi za filamu zimekuwa zikikatwa kodi zaidi ya mara tatu na kuuita huo ni uonevu kwao.

Naye, John Lisa alisema ipo haja ya serikali kuangalia namna gani itakuja na sera ya filamu kwa sababu licha sekta hiyo kukua lakini haitambuliwi kama ajira rasmi.

Mwandaaji Husna Posh maarufu Dotnata, alisema wamekuwa wakiumia na gharama za uandaaji wa filamu lakini maumivu yake wamekuwa wakiugulia kimya kimya kwa sababu wakisema wanunuzi wao watawasusia.



KOCHA wa Tennis, Ismail Said, akimvalisha medali, Nayfat Badru ambaye aliibuka mshindi wa kwanza katika mashindano ya Kijitonyama JuniorTennis Tournament chini ya miaka 12, yaliyofanyika katika viwanja vya Kijitonyama jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Jux kusaidia muziki wa asili Kahama

**Na Shaban Njia, KAHAMA**

MSANII wa Bongo Fleva, Juma Musa maarufu Jux anatarajia kukutana na wasanii wa ngoma za asilia wilayani Kahama mkoani Shinyanga ili kuangalia namna ya kuwasaidia na kukuza muziki huo.

Hayo yalibainishwa jana na Mkurugenzi wa Arbab MB Entertainment and African Boy, Mbwana Imamu wakati akizungumza na vyombo vya habari juu ya ujio wa Jux wilayani hapa katika tamasha linalojulikana kwa jina la "Jux live in Kahama" na litakalofanyika Julai 30 mwaka huu.

Alisema kuwa, waandaji wengi wa matamasha hivi sasa wamekuwa wakitumia miziki ya kizazi kipya kuwaburudisha wananchi, hali ambayo inafanya miziki ya asili kutokupendwa na wasikilizaji.

"Mimi katika uandaaji wangu wa nyimbo za kizazi kipya sijawahi kuhusika na uandaaji wa ngoma na muziki wa asili, hili nitalichukua na kulifanyia kazi na nitaanza nalo kwa kiasi kikubwa na wasanii wa ngoma za asilia wa Tanga ambako ndiko natokea," alisema Imamu.

Aliongeza kusema, Jux anampango wa kuibua vipaji vya ngoma za asili zinazopigwa pembezoni mwa vijiji ili na wao waweze kutamba katika matamasha mbalimbali hapa nchini.

# Simba Queens kupaa kesho kwenda Kenya

**Na Saada Akida**

KIKOSI cha Mabingwa wa Ligi Kuu Soka la Wanawake Tanzania, Simba Queens kinatarajiwa kuondoka nchini kesho kuelekea Kenya katika michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika ya wanawake kanda ya Baraza la vyama vya Soka Afrika Mashariki na Kati (CECAFA).

Akizungumza na gazeti hili jijini jana, kocha wa kikosi hicho Mussa Hassan 'Mgosi' alisema maandalizi ya safari yamekamilika na wanatarajia kuondoka nchini kati ya Jumanne au Jumatano kulingana na majibu ya vipimo vya COVID-19 vitakapokamilika.

Alisema wamejiandaa vizuri kwa ajili ya kuipa heshima Simba kwa kufuata nyayo za kaka zao katika kufanya vizuri zaidi katika michuano ya kimataifa.

**"Mipango yetu kuelekea Kenya mapema sana ili kuzoea hali ya hewa kwa sababu tumesikia ni baridi sana, hali hiyo mipango yetu ni kuondoka hapa Jumanne kama vipimo vya COVID 19 vikiwahi kutoka, kama vitachelwa tunaweza kuondoka Jumatano," alisema Mgosi.**

"Tumejiandaa vizuri na tayari tumewaona na kupata taarifa za wapinzani wetu ambao tuko nao kundi mmoja, tunatarajia kwenda kufanya vizuri na kuhakikisha tunakuwa miongoni mwa timu zitakazokwenda Misri," alisema Mgosi.

Alisema kulingana na maandalizi yao wanaenda Kenya kupambana katika kila mechi ili wafanye vizuri na wafikie malengo yao ya kuwa mmoja ya timu ambayo itaenda nchini Misri kushiriki Ligi ya Mabingwa ya soka Afrika kwa Wanawake.

Simba Queens imepangwa kundi A zikiwa ni timu Lady Doves WFC ya Mabingwa wa Uganda na PVP FC ya Burundi, ambao watashiriki michuano hiyo itakayoanza Julai 17, mwaka huu nchini Kenya.

# MANULA MKALI WA 'CLEAN SHEETS' LIGI KUU

**Na Adam Fungamwango**

GOLIKIPA namba moja wa Simba na Timu ya Taifa, Taifa Stars, Aishi Manula anaongoza kwa kucheza mechi 17 kwenye Ligi Kuu bila kuruhusu wavu wake kuguswa maarufu kama 'clean sheets'.

Kwa mujibu wa takwimu za Ligi Kuu, Manula ambaye timu yake ya Simba imebakisha mechi tatu kwenye ndiye kipa atakayemaliza Ligi Kuu msimu wa 2020/21 akiwa na 'clean sheets' nyingi kutokana na makipa wote waliobaki timu zao kubakisha mechi mbili tu.

Kutokana na hali hayo hakuna uwezekano wa kipa yoyote kumpiku Manula msimu huu, kwani wakiwa wanaomfuatia wana 'clean sheets' 13 tu.

Makipa hao ni Metacha Mnata wa Yanga ambaye kwa sasa amesimamishwa na klabu yake kutokana na madai ya utovu wa nidhamu na Aboutwalib Mshery wa Mtibwa Sugar na Haroun Mandanda wa Mbeya City.

Makipa wengine ambao wana 'clean sheets' nyingi kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo ipo ukingoni kabisa ni Jeremiah Kisubi wa Prisons ambaye amedaka mechi 12 bila kuruhusu bao.

Kipa mkongwe wa KMC, ambaye anaidakia timu ya taifa, Taifa Stars, Juma Kaseja, yeye ana 'clean sheets' 11, akiwa na kipa Aron Kalambo wa Dodoma Jiji.

Golikipa wa Biashara United, Daniel Mgore ni miongoni mwa makipa waliong'ara msimu huu, akicheza mechi 10 bila kuruhusu wavu wake kutikisika.

# Michezo

Jumatatu Julai 12, 2021

Nipashe




## Messi: Nimesubiri sana kubeba taji na Argentina

HABARI UK. 22



Wachezaji wa Timu ya Taifa ya Argentina wakiongozwa na nahodha wao Lionel Messi, wakifurahia kombe la michuano ya Copa Amerika 2021 walilolitwaa juzi usiku baada ya kuifunga Brazil bao 1-0, katika Uwanja wa Maracana. **PICHA: MTANDANO**

# YANGA YAELEKEZA NGUVU FAINALI FA

### ●●● Uongozi wajipanga kupeleka kilio kingine Msimbazi, kocha na wachezaji...

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Yanga umesema umejipanga vizuri kwa ajili ya mchezo wa Fainali ya Kombe la Shirikisho la soka Tanzania, TFF, kwa kuwafunga Simba kwa mara nyingi, Julai 25, kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika, Kigoma.

Akizungumza na gazeti hili, Kaimu Katibu Mkuu wa Yanga, Haruna Mfikirwa alisema wamejipanga zaidi kumpatia ushirikiano wa kutosha kocha Nesreddine Nabi kwa kila atakalokuwa anahitaji.

"Mipango yetu ni kuhakikisha tunakuwa na Yanga imara kuanzia kwa wachezaji mpaka maeneo mengine yote kulingana na mipango yetu na hilo linawezekana hasa kuanzia mchezo wa fainali kuhakikisha tunafanya vizuri na kutwaa ubingwa," alisema Mfikirwa.

Alisema viongozi wana imani na wachezaji na benchi la ufundi kwa kuendelea kufanya vizuri katika michezo iliyobakia ya Ligi Kuu Bara pamoja na mchezo wa fainali kutwaa taji hilo.

Alisema endapo watakosa ubingwa wa Ligi Kuu watapambana kuhakikisha wanabeba taji la FA.

Naye Kocha Mkuu, Nesreddine Nabi alisema wachezaji wake wamekuwa wavumilivu na kufanikiwa kwa kiasi kikubwa kupokea mazoezi ya nguvu ambayo husaidia kutengeneza miili yao kuwa tayari kushindana muda wote.

"Wachezaji wangu kiufundi wameimarika tunapokuwa na mpira na hata wakati hatuna tunautafuta kwa nguvu na tukiupata tunautunza," alisema.

Aliongeza kusema kuwa ameona mabadiliko na muunganiko mzuri wa kikosi kwa wachezaji na wanapambana kutafuta matokeo mazuri katika michezo iliyosalia na huku akihitaji kuendelea kufanya vizuri katika mchezo wao fainali dhidi ya Simba.

## BODI YA LIGI YASOGEZA MECHI KWA SIKU MOJA

**Na Saada Akida**

BODI ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB) imesogeza kwa siku moja mbele michezo yote ya mzunguko wa 33 wa Ligi Kuu ambayo kwa sasa itachezwa Julai 15, 2021 badala ya Julai 14 ilivyotangazwa awali.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Idara ya Habari na Mawasiliano ya Bodi ya Ligi, mabadiliko hayo yametokana na ombi la timu ya Polisi Tanzania kusogeza angalau siku moja mbele mchezo wao wa ligi hiyo dhidi ya Kagera Sugar.

Maombi hayo ni baada ya timu hiyo yenye maskani makuu mjini Moshi, kupata ajali ya barabarani Julai 9 iliyosababisha majeraha kwa baadhi ya wachezaji wao.

"Ili kupata uwiano sawa wa michezo kuelekea kumalizika kwa msimu, Bodi ya Ligi imeamua kusogeza michezo yote ya mzunguko wa 33 kwa siku moja mbele, hivyo timu zote zitacheza mechi za mzunguko huo Julai 15 kama ilivyoelezwa hapo juu."

"Tunawatakia nafuu ya mapema wachezaji na maofisa wote wa Polisi Tanzania FC waliopata majeraha katika ajali hiyo na kila la kheri kwa timu zote katika maandalizi ya kuelekea michezo iliyosalia ya ligi hiyo," ilisema taarifa hiyo.

Mbali na mechi ya Polisi Tanzania dhidi ya Kagera Sugar, utakaochezwa, Ushirika Moshi, michezo mingine inayotakiwa kucheza Julai 14, 2021 ni Tanzania Prisons dhidi ya Biashara United utakaopigwa katika dimba la Nelson Mandela, Rukwa.

KMC FC dhidi ya JKT Tanzania huo utachezwa uwanja wa Uhuru saa 8:00 mchana, Yanga dhidi ya Ihefu FC, dimba la Benjamin Mkapa saa 10:00 jioni na Azam FC ikiwakaribisha mabingwa wapya kwa msimu wa nne mfululizo, Simba, Uwanja wa Azam Complex, saa 1:00 usiku.

Katika viwanja vingine kutakuwa na mechi ya Ruvu Shooting dhidi ya Namungo FC, katika dimba la Mabatini, Pwani, Mbeya City dhidi ya Gwambina FC wakiwa ugenini, uwanja wa Sokoine, jijini Mbeya.

Dodoma Jiji FC watakuwa nyumbani ikiwakaribisha Mtibwa Sugar katika Uwanja wa Jamhuri, Dodoma na Coastal Union ikiwa nyumbani ikitafuta pointi tatu muhimu dhidi ya Mwadui FC.

9 770856 541002

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042